

Mwongozo wa Utamaduni Toleo la Kwanza

Kubadilishana Tamaduni
za Kijerumani na za Kitanzania



Limeandaliwa
na

Anna Hoppenau, Johannes Hahn, Oliva Lyimo na Lisa Bendiek
German-Tanzanian Partnership (DTP) and Tanzania Youth Coalition (TYC)

Yaliyomo:

Somo	Ukurasa
Utangulizi.....	3
Utamaduni ni Nini?	4
Changamoto zilizomo katika Mawasiliano ya Tamaduni.....	4
Dhana ya Wakati: Linearism and Circularism	6
Dhana ya Jamii: Ubinafsi and Umoja	7
Tofauti za Tamaduni Duniani	8
“Viungo vya Utamaduni“	9
Mifano: Kulinganisha Tamaduni za Ujerumani na Tanzania.....	11
Mshtuko katika Utamaduni: Jinsi ya Kukabiliana nao na Nafasi yake	12
Sababu za Ubaguzi na Ukandamizaji	14
Jinsi ya Kujibadili Kitamaduni na Mapungufu Yake.....	15
Zana zinazotumika kwenye Mawasiliano ya Tamaduni na Ushirikiano.....	16
Kurasa za Nyongeza	
Tunamaanisha nini tunapozungumzia utamaduni?.....	17
Maana mbalimbali za utamaduni kama zilivyofafanuliwa na Chuo Kikuu cha Manitoba	18
Mtindo wa Utamaduni wa Iceberg	21
Utamaduni wa Albatros - Zana ya Kuiga.....	22
Utamaduni na Migogoro	23
Mapendekezo.....	28
Marejeo	28

Utangulizi

Mwongozo huu wa utamaduni umeandaliwa na Deutsch-Tansanische Partnerschaft e.V. (Asasi ya Ushirikiano wa Ujerumani na Tanzania, DTP) kwa kushirikiana na Tanzania Youth Coalition (Ni shirika la vijana Tanzania linalojumuisha mashirika madogo ya vijana wa Kitanzania (TYC). DTP ni Asasi isiyo ya kiserikali ya Ushirikiano baina ya Ujerumani na Tanzania ambayo makao yake makuu yapo Ujerumani na limekuwa likishughulika na shughuli zote zinazohusu nishati mbadala na majiko nchini Tanzania tangu mwaka 2001. Mshirika wa DTP's nchini Tanzania ni Shirika la Vijana Tanzania (TYC). Asasi hizi mbili zimekuwa zikishirikiana katika mpango wa kujitolea kubadilishana unaoitwa "worldwards - ambao madhumuni yake ni kubadilishana tamaduni na kutunza mazingira nchini Tanzania" ambao huwawezesha Wajerumani 16 kuja Tanzania kufanya kazi za kujitolea kila mwaka, pamoja na kutoa fursa kwa Watanzania kwenda Ujerumani na wengine hapa Tanzania kufanya kazi za kujitolea. Tangu mwaka 2002 Wajerumani vijana hutumwa nchini Tanzania kufanya kazi za kujitolea katika miradi ya mazingira na tangu mwaka 2008 pia vijana wa Kitanzania wawili huenda Ujerumani kufanya kazi za kujitolea. DTP hupanga mpango wa ubadilishanaji nchini Ujerumani na TYC ni Asasi ya kizawa ambayo huratibu mpango huo hapa Tanzania.

Mpango huu wa kujitolea umewapa fursa vijana kupata uzoefu wa ubadilishanaji wa tamaduni kwa kufanya kazi na watu wenye asili tofauti ya tamaduni. Lengo letu hasa ni kuongeza uelewa wa tamaduni na kulinda mazingira kwa njia ya kufanya kazi katika nyanja za nishati mbadala.

Kwetu sisi kuelewana kimataifa maana yake ni kuheshimu tamaduni nyingine, na kujifunza kutoka kwa kila mmoja kwa kufanya kazi na kila mmoja wetu. Hivyo, dhana ya mawasiliano katika tamaduni ina umuhimu mkubwa katika mradi wetu.

mwongozo huu uliandaliwa ili kuwezesha namna ya kupambana na changamoto zilizomo katika mawasiliano ya tamaduni. Mwongozo huu haukuandaliwa ili kutoa majibu rahisi kwa mtindo wa "Ujerumani iko namna hii, Tanzania iko namna hii", bali kutumika kama chombo cha kuchunguza tofauti ya tamaduni zetu.

Mwongozo huu unaweza ama utumike katika mambo haya yafuatayo na si vinginevyo:

- (i) Semina ya maandalizi kwa ajili ya mradi wa Kusini na
- (ii) Kaskazini { South North Program} kwa vijana wa Kitanzania wanaokwenda Ujerumani kufanya kazi za kujitolea (ambayo huandaliwa na Tanzania Youth Coalition (TYC)
- (iii) Semina kwa ajili ya Viongozi wa vituo wanaohusika na miradi (ambayo huandaliwa na Michael Onesimo, Mshauri wa Miradi ya Vijana wanaofanya Kazi za Kujitolea wa DTP na TYC)
- (iv) kwa ajili ya maeneo ya wenyeji yanayohusika na mradi nchini Tanzania, ambako vijana kutoka Ujerumani wanaofanya kazi za kujitolea watatumia.

Jambo la kuzingatia: Mwongozo huu wa Utamaduni pia una kurasa nyingine zenye ufafanuzi wa kazi nyingine nyingi za ziada. Hivyo wanaweza kukusaidia kuandaa warsha au semina zinazohusu masuala ya tamaduni. Kitu cha muhimu ni kuwa wabunifu!

Utamaduni ni Nini?

"Mfumo wa pamoja wa kiimani, maadili, desturi, tabia, na kazi za sanaa ambao hutumiwa na wanajamii katika kukabiliiana na dunia na kati ya mtu mmoja na mwingine, na kwamba hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya kujifunza1"

"Katika Karne ya Ishirini, "utamaduni" umetumika kama dhana iliyo kati ya anthropolojia, ambayo inajumuisha mambo yote ya binadamu ambayo si matokeo ya kurithishana2".

Hizi fafanuzi mbili za maana ya utamaduni zinaonyesha kwamba utamaduni upo kila mahali na ni kila kitu!

- (i) Hujengwa kwa njia ya historia
- (ii) Hujumuisha kanuni zote za maadili, dhana ya ubinadamu, dhana ya wakati
- (iii) Hutuwezesha kuifahamu, kutafsiri na kuielewa dunia inayotuzunguka kwa namna mbalimbali
- (iv) Huonyeshwa katika shughuli za kijamii, mazungumzo kati yetu, lugha, kiroho, katika mlolongo mzima wa maisha yetu
- (v) Husonga mbele daima, unajiendeleza wenyewe na kukua
- (vi) Ingawa utamaduni unaweza kutazamwa kwa upana kama mali ya jamii, huonyeshwa na mtu mmoja mmoja, na tusiupe mtazamo wa pamoja!

Hitimisho: ***Utamaduni hutengeneza utambulisho wa mwanadamu.***

(Kwa maelezo zaidi tazama kurasa za nyongeza ya 1 - 2)

¹ www.umanitoba.ca/faculties/arts/anthropology/courses/122/module1/culture.html

² <http://en.wikipedia.org/wiki/culture>

Changamoto zilizomo katika Mawasiliano ya Tamaduni

Mawasiliano ya tamaduni yanakabiliwa na changamoto nyingi kwa namna mbalimbali. Tamaduni mbalimbali zimejengwa katika viwango tofauti. Na hii ndiyo sababu tuifahamu na kuitafsiri dunia iliyotuzunguka tofauti na kwa namna mbalimbali.

Mtu anaweza kusema kuwa sisi wote tumevaa "miwani ya utamaduni": Ni dunia ya aina moja tunayoina lakini katika rangi au mwanga tofauti. Hatuwezi kujitolea kubadilishana miwani ya tamaduni zetu kwa sababu tumekuzwa katika tamaduni fulani ambazo zimetengeneza utambulisho wetu na kutufanya tuishi kwa namna ya miwani ya tamaduni hizo za pekee. Lakini tunaweza kujaribu kuangalia sehemu zote kupitia miwani hiyo, tunaweza kujaribu kuelewa ni kwa jinsi gani mtu aliyevaa miwani mingine anavyoelewa ulimwengu. Na kwa kipindi fulani miwani yetu inaweza kubadilika rangi kidogo. ... Hii ni maana ya kuelewana katika tamaduni.

Kutokana na kutofatiana kwa tamaduni zetu, kutokuelewana kati ya watu wa jamii moja na nyingine hutokea kirahisi. Mara nyingi hivi hutokea na hatutambui wala kuona kama ni kutokuelewana kwa sababu tumefungamana kifikra na tamaduni zetu na hatuoni kama wengine wanafikiri kwa namna tofauti hivyo wanaweza kuwa na mashaka au kusumbuliwa na tabia zetu au kwa tutakayoyaongea.

Hata mambo ya msingi hufanyika kwa njia tofauti au kufasiriwa tofauti. Tamaduni mbalimbali zina tabia tofauti, namna ya kufikiri, namna ya kufanya mabo yenye maana, na namna ya kutatua migogoro.

Vile vile, njia na sheria za mawasiliano hutofautiana. **Njia za mawasiliano hujumuisha lugha, tabia na sheria za namna ya kushirikiana na watu wa jamii nyingine na maadili yao kwa jumla.**

Kwa mfano, nchini Tanzania imezoeleka kumsalimia mtu aliyekuzidi umri "Shikamoo", kwa sababu watu wazima wanatakiwa kupewa heshima na walio wadogo. Nchini Ujerumani mtu aliyekuzidi umri huamkiwa pia kwa namna fulani ambayo pia huonyesha heshima kwa mtu aliyekuzidi umri, hakuna salamu maalum.

Vile vile, siku hizi nchini Ujerumani wazazi hukosolewa mara nyingi moja kwa moja na watoto wao. Hii ni tofauti na nchini Tanzania, kwa sababu kuna namna nyingine ya kukosoana na kushughulika na uhusiano kati ya watoto na wazazi.

Hii ni mifano michache inayoonyesha tofauti ya mawasiliano katika nchi kama Ujerumani na Tanzania kwa sababu ya tofauti chache zilizopo katika asili ya tamaduni mbalimbali.

Lakini kutokuelewana huku hakutokei kupitia mawasiliano ya moja kwa moja, bali pia kupitia mawasiliano yasiyo ya moja kwa moja na mawasiliano yasiyo na ishara.

But misunderstandings do not only happen through direct communication, but also through **indirect communication or nonverbal communication**. Moja ya misemo maarufu katika nyanja hii huu:

"Hatuwezi kutowasiliana"

Hii ina maana tunawasiliana daima hata kama si kwa kuongea. Kwa ufafanuzi zaidi soma " Mfumo wa Utamaduni wa Iceberg " ambao utaupata katika sura ya mwisho ya Mwongozo ambayo ni kurasa 3 katika sehemu ya "Taarifa Zaidi".

Kwa mfano: Nchini Tanzania rafiki anaweza kukushika mkono wako kwa muda mrefu wakati mnazungumza lakini si ya kawaida nchini Ujerumani ambako mtu hukusalimia kwa kukushika mkono mara moja tu tena haraka, wakati wanandoa hushikana mikono au marafiki wa karibu sana humkumbatiana. Pia nchini Ujerumani ni kawaida watu kushikana mikono kwa muda mfupi na kwa nguvu wakati nchini Tanzania watu hushikana taratibu. Kwa hiyo, mtu ambaye hana mazoea ya kushikana mikono wakati anazungumza hali hii inaweza kumkosesha raha pia ambaye ana mazoea hayo anaweza kukosa raha kwa kutobadilishana ishara hii rahisi.

Kumbuka kwamba hakuna ambacho ni sahihi au si sahihi katika tofauti za kitamaduni, ni tofauti tu! Ingawaje tathmini daima haziwezi kuepukika, lengo letu si kukosoa haraka haraka, bali ni kujaribu kutazama hali hiyo kwa upande tofauti. Tunaweza kufikia lengo hili lakini na si kwa kutazama haraka haraka, bali kuchunguza kwanza, kufafanua, na mwisho kutoa uamuzi.

Na kama hatuyatili maanani haya yote, pengine tunaweza kutoelewana na watu wa tamaduni nyingine. Kwa ajili ya kufanya kazi na kuishi pamoja kwa amani katika dunia hii ya utandawazi ni muhimu tukaacha kutokuelewana. Kwa hiyo ni muhimu sana iwapo tutaboresha ujuzi wetu wa mawasiliano ya tamaduni. Utafaidika sana ukijaribu kuutazama ulimwengu kwa kutumia miwani tofauti, na tunaamini kuwa ni hatua ya moja kwa moja na yenye ufanisi kwa mtu mmoja mmoja akijaribu kuendeleza zaidi mawasiliano ya tamaduni na hatimaye kuleta uelewano na heshima.

(Kwa maelezo zaidi tazama kurasa za nyongeza ya 3)

Dhana ya Wakati: Linearism and Circularism

Tamaduni mbalimbali mara nyingi hutokana na dhana tofauti za nyakati. Dhana hizi huamua shughuli zote za kijamii, utendaji kazi, namna ya kuishi, n.k. Hivyo kwa kufanya kazi kwa pamoja na mwanajamii kutoka tamaduni tofauti, ni kuelewa jambo hili. Utamaduni wa Tanzania ni wa dhana ya wakati ya 'circular' na utamaduni wa Ujerumani ni wa dhana ya wakati ya 'linear'.

<i>Imani za tamaduni za ndani, maadili yaliyojificha, sababu za tabia</i>	CIRCULARISM	LINEARISM	<i>Imani za tamaduni za ndani, maadili yaliyojificha, sababu za tabia</i>
<i>tamaduni zinazoji- onyesha, matendo, tabia</i>	Wakati huzunguka Wakati hujirudia Usiku ukipita, siku mpya huanza Fanya mambo mbalimbali kwa mara moja, Hairisha kazi ("labda kesho") Mawasiliano na kushirikiana na wenzio ni muhimu zaidi kuliko kupangilia muda Huwezi kupoteza muda kwa sababu upo daima mikutano hubadilishwa kirahisi, iwapo mtu atachelewa, msubiri. Kushirikiana hasa ndilo jambo la muhimu	Wakati hunyooka Wakati hupita Siku ikipita, imekwisha Fanya jambo moja baada ya jingine, "malizia shughuli Ratiba ni muhimu Muda ni mali, huweza kupotea Wakati hutengeneza mpangilio wa maisha ya kila siku na uhusiano na binadamu wengine Kuwahi, tengeneza ratiba na kuzifuata, fanya mambo haraka	<i>tamaduni zinazoji- onyesha, matendo, tabia</i>
<i>Tafsiri, maamuzi yatolewayo na watu wengine</i>	Mahusiano, salamu huchukua muda mwingi, uchelewaji, mambo hufanyika kwa kuchelewa (au hakuna kabisa) "hakuna uhakika", "kutoheshimu kazi", "hakuna kipaumbele katika shughuli", "usimamizi mbaya"	"harakisha", "usahihi binafsi", hakuna uungwana", "hakuna heshima kwa mtu"	<i>Tafsiri, maamuzi yatolewayo na watu wengine</i>

Ukitazama tamaduni zote mbili, wa Ujerumani na Tanzania, ni wazi kuwa utaona wakati unasonga mbele. Lakini mtu anaweza kusema kwamba wakati nchini Ujerumani hii hutokea katika mstari ulionyooka, nchini Tanzania ni tofauti kwani badala yake inazunguzunguka!

Dhana ya Jamii: Umoja na Ubinafsi

Kama ilivyo kwamba tamaduni za Tanzania na Ujerumani hutofautiana katika suala la dhana ya muda, pia hutofautiana katika suala la dhana ya jamii.

Umoja ni neno linalotumiwa kuelezea maadili yoyote, ya kisiasa au mtazamo wa jamii, na hutumika kuisitiza kutegemeana kwa binadamu na umuhimu wa umoja badala ya umuhimu wa kila mtu mmoja mmoja. Watu wanaojali umoja huzingatia jamii, na mara nyingi huyapa kipaumbele malengo ya kikundi kuliko malengo ya mtu binafsi³.

Ubinafsi ni neno linalotumiwa kuelezea maadili yoyote, ya kisiasa au mtazamo wa jamii, na hutumika kuisitiza kutegemeana na kujitegemea. Watu wanaojali ubinafsi huihua utekelezaji wa matakwa na malengo ya mtu mmoja mmoja wakati huo huo wakipinga kuingiliwa na watu au mawazo kutoka nje katika uchaguzi wa mambo yao, iwe kutoka kwa jamii, au kikundi chochote au taasisi⁴.

Kama unaweza kuhisi kirahisi, utamaduni wa Tanzania ni wa umoja na utamaduni wa Ujerumani ni wa ubinafsi.

Mifano:

Umoja	Ubinafsi
Watu huzaliwa katika familia kubwa; familia hutunza wanachama wake na kutarajia uaminifu kutoka kwao	Kila mtu hukua kutunza watoto na mwenz wake tu
Mara zote unatakiwa uwe mwenye amani na uepuke malumbano ya moja kwa moja	Utaonekana jasiri na mkweli iwapo utaongea unachofikiri na kutoa msimamo wako
Kupata kazi au kupanda cheo hutegemea wenzio na ni namna gani unakubalika	Kupata kazi au kupanda cheo hutegemea sifa ulinazo
Mahusiano ni muhimu zaidi ya kazi	kazi ni muhimu zaidi ya mahusiano
Mchakato wa kazi ni muhimu zaidi kuliko matokeo yake	Matokeo ya kazi ni muhimu zaidi kuliko mchakato wake
Maisha binafsi hushirikisha familia, jamii, n.k.	Kila mtu ana haki ya kuwa na faragha katika maisha yake
Sheria na kanuni hutegemea wewe ni wa kundi gani	Sheria na kanuni ni sahihi kwa kila mtu kwa namna moja
Maelewano na makubaliano katika jamii ni malengo muhimu	Kutosheka kwa kila mtu mmoja mmoja ni lengo muhimu

³ <http://en.wikipedia.org/wiki/Collectivism>

⁴ <http://en.wikipedia.org/wiki/Individualism>

Tofauti za Tamaduni Duniani

lfuatayo ni orodha ya mifano inayoonyesha tofauti za tamaduni duniani kote, ikilinganisha kwa kutegemea ukomo wa madaraka, wajibu wa mwanaume na mwanawake na kuepuka hali ya kutokuwa na uhakika. Orodha hii imetokana na "Mfumo wa Kutathmini Tamaduni" kama ulivyoelezewa na Geert Hofstede. Somo la mwisho ambalo ni umoja na ubinafsi pia liko katika mfumo wa Hofstede.

Ukomo wa Madaraka

Ukomo wa Mwenye Mamlaka Makubwa	Ukomo wa Mwenye Mamlaka Madogo
Matabaka na kukosekana kwa usawa wa kijamii huonekana ni kitu kibaya na ni lazima iondolewe	Matabaka ni kitu cha kawaida, hukubalika na ni kitu kizuri
Wazazi huchukulia watoto wao kama watu binafsi na huheshimu maoni yao	Wazazi hulea watoto wao na kuwafanya wawaheshimu na kuwatii wazazi
Walimu hutarajia wanafunzi wao kuwa mstari wa mbele kutekeleza mipango	Mpango siku zote hutekelezwa na mwalimu
Wafanyakazi hupenda kuulizwa wakati wanafanya maamuzi	Wafanyakazi hutegemea kupewa maagizo ya nini cha kufanya
Upendeleo kwa watu fulani/ vikundi huonekana ni jambo baya	Upendeleo (kwa mfano kwa mameneja) ni kitu cha kawaida na kinakubalika
Matumizi ya nguvu ni lazima yaidhinishwe. Watu hutathmini uongozi si kwa kiasi cha mamlaka yaliyotumika bali kiasi gani imetenda haki au imekosea	Nguvu ni muhimu zaidi ya haki au makosa. Kiongozi ana mamlaka ambayo ana uwezo wa kuyatumia au la
Mamlaka aliyonayo mtu hutegemea wadhifa wake, The power a person has depends on the status, maarifa, uwezo wa kuwatumikia wengine	Mamlaka aliyonayo mtu hutegemea familia, marafiki na uwezo wa kuwaadhibu watu wengine

Mwanaume/Mwanamke


Mwanamke	Mwanamume
Muhimu: anavyohudumia wengine, anavyoilinda jamii kimaadili	Muhimu: Mafanikio ya kipato na maendeleo
Anafanya kazi ili aweze kuishi	Anaishi ili aweze kufanya kazi
Kijamii na Serikali	Ushindani

Kuepuka hali ya kutokuwa na uhakika/salama

Weak avoidance of uncertainty	Strong avoidance of uncertainty
Hali ya kutokuwa na uhakika/salama ni kawaida na inakubalika katika maisha	Hali ya kutokuwa na uhakika/salama ni tishio na watu hujaribu kupambana nayo kwa uwezo walionao
Kamwe hutakiwi kuonyesha uchokozi au hisia zako	uchokozi na hisia huweza kuonyeshwa katika mazingira yanayokubalika
Students like long discussions with open end	Students like simple questions and clear answers
Mwalimu anaweza kusema 'sijui'	Mwalimu anatakiwa aweze kujibu kila kitu
Watu hupenda kupumzika; na hufanya kazi kwa bidii inapobidi tu	Watu wana ari na bidii ya kufanya kazi
Hakuna haja ya kanuni/sheria mpaka zinapohitajika	Watu wanahitaji kanuni/sheria, hata kama kamwe hawatafanya kazi
Kama hatuwezi kufuata kanuni/sheria, inabidi kanuni/sheria zibadilishwe	Kama hatuwezi kufuata kanuni/sheria, tuna makosa na inabidi tujirekebishe wenyewe

“Kitunguu/Kiungo cha Utamaduni”


Mfumo mmoja wa mfano ambao unaweza kuonyesha taswira ya namna maadili yanavyoambatana na kila tendo ni “Kitunguu/Kiungo cha Utamaduni”, hebu angalia, pia ni chombo kikubwa kinachotumika kuchambulia:



Maelezo: Tafsiri ya tamaduni kwa kawaida hutokana na vitu vinavyoonekana kwa juu, katika uchunguzi tunaofanya, tofauti tunayoona kati ya utamaduni wetu na utamaduni wa wenyeji, na ni lengo kubaki katika sehemu zinazoonekana kwa juu lakini pia tunahitaji kufahamu thamani ambayo huambatana nayo.

Ndiyo maana “tunachunguza kwa ndani” kwenye kiini cha kitunguu, ambacho huwasilishwa katika magamba yaliyojipanga katika safu tofauti za mduara kama ilivyo katika picha. Ukianza kuchunguza kuanzia safu ya juu kabisa, utatoka katika sehemu inayoonekana na kwenda sehemu isiyoonekana, na ndipo utagundua sehemu zinazotakiwa kuondolewa, na kwamba inabidi kuwa makini kufahamu sehemu zote mpaka kwenye kiini na ndipo utaweza kupata maelezo juu tabia fulani.

Ufuatao ni mchoro unaoonyesha mfano wa kitunguu cha utamaduni kinavyonyesha tofauti moja ya mawasiliano kwa kitanzania na kwa kijerumani.



Hii ni baadhi ya mifano michache ambayo inaonyesha utamaduni wa Tanzania na Ujerumani katika hali tofauti:


Tanzania	Ujerumani
<u>Namna ya kushughulika na migogoro:</u>	
Unatakiwa uwe mtu wa amani na uepuke malumabno ya moja kwa moja. Kama utatokea mgogoro kati ya pande mbili, ni muhimu sana mkielewana kuliko kulaumiana kila mmoja kwa makosa yake.	Kujieleza unavyofikiri na kusemezana na mwenzio inaonekana ni jambo la kishujaa na la kweli. Kukosoana moja kwa moja ni kawaida. Kama mtu amefanya jambo ambalo linaonekana ni kosa, inambidi awajibike.

Tanzania	Ujerumani
<u>Namna ya kushughulika na muda:</u>	
<p>“Pole pole”. Muda hutawaliwa na watu, watu hawataliwi na muda. “Kesho kutwa” haina maana ya kesho tu, bali pia muda usiojulikana siku za mbeleni.</p>	<p>Kwa kawaida, kuchelewa hata kwa dakika moja huhesabika kama ni kuchelewa sana. Taratibu mara nyingi hushughulikiwa kwa makini sana. Daima muda hukimbia, watu si tu wanapanga ratiba ya kazi zao, bali pia muda ambao wako huru.</p>
<u>Namna ya kushughulika na watu wenye umri mkubwa:</u>	
<p>Watu wenye umri mkubwa katika jamii ni watu wa kuheshimiwa, na husalimiwa “Shikamoo”. Watu wenye umri mkubwa huonekana kuwa wenye maarifa makubwa kwa sababu ya uzoefu wao. Kwa ujumla, mila huonekana ni muhimu sana kwa Watanzania.</p>	<p>Unaweza kumsalimia mtu mwenye umri mkubwa kwa namna fulani ya heshima (kwa kutumia neon linaloonyesha wingi “Sie”) na ambayo ni rasmi, lakini vijana wa sasa hivi watu wenye umri mkubwa hawaonekani kama ni watu wa kuheshimiwa kuliko wengine. Kwa ujumla, umuhimu zaidi hupewa ubunifu kuliko mila.</p>
<u>Namna ya kushughulika na wageni:</u>	
<p>Kama wewe ni mgeni nchini Tanzania watu wengin watakaribisha na unaweza kuwa raifki yao kirahisi. Hata kama unaelekea dukani, watu watakuuliza maswali, wanapenda kukufahamu, wanakufuata na wanataka kukusaidia. Watu hupenda kujichanganya siku nzima.</p>	<p>If you are new to Germany, it takes a long time for you to befriend people. They are dealing with their own businesses and rarely come up to strangers. People only call others their real friends after they know each other for a very long time. At the beginning people tend to keep distance.</p>
<u>Namna ya kushughulika na dini/mambo ya kiimani:</u>	
<p>Dini ni sehemu muhimu katika maisha, karibu kila mtu hujiona mtu wa kidini. Kwa upande mwingine, ni mara chache sana suala la dini huchukuliwa kama si jambo la kawaida; kuna historia ndefu ya kuwepo kwa ushirikiano wa amani. Watu wa dini tofauti hawaonani kama vikwazo bali huonekana kama watu wa kukuimarisha kiimani, na mifarakno ya kidini ni michache.</p>	<p>Wajerumani wengi hawana dini kabisa. Hivyo sehemu za kidini kama vile makanisa mara nyingi ziko tupu hazitembelewi, na wakati mwingine huonekana kama “mambo ya kizamani”. Watu wa dini tofauti wakati mwingine huwaona wale wa dini nyingine kama vikwazo na wanakuwa na hisia za uadui. Migogoro ya ndani ya kidini hutokea mara kwa mara.</p>
<u>Namna ya kushughulika na nini wajibu wa mwanamke au wa mwanamume:</u>	
<p>Katika mahusiano na maisha ya kila siku kuna desturi ya namna mwanamume na mwanamke watakavyoshirikiana. Wanaume mara nyingi wanatawala kuliko mwanamke. Ndoa za wake wengi ni halali.</p>	<p>Jinsi muda unavyopita, majukumu ya kijinsia yanatoweka na wanawake wanazidi kuwa sawa na wanaume, katika Nyanja zote za binafsi na sehemu za kazi. Karibu theluthi moja ya ndoa “zinavunjika”. Majukumu ya kijinsia yanapotea na ndoa za jinsia zinazidi kuhalalishwa. Ndoa za wake wengi ni halali.</p>

Mshtuko katika Utamaduni: Jinsi ya Kukabiliana nao na Nafasi yake

"Mshtuko katika Utamaduni" ni hali ya wasiwasi na hisia (mshangao, kuchanganyikiwa, wasiwasi, n.k.) inayojitokeza wakati watu wanatakiwa kufanya kazi katika mazingira mapya kiutamaduni au kijamii, kama vile katika nchi ya kigeni. Huzidi kujitokeza jinsi ugumu wa namna ya kujizoeza utamaduni mpya unapojitokeza na kusababisha matatizo katika kujua nini ni sahihi ama si sahihi. Mara nyingi hii huambatana na kuchukua au hata kutokubaliana (maadili au sanaa) na mambo fulani fulani ya utamaduni huo mpya⁵.

Mabadiliko katika utamaduni ni jambo lisiloisha, ni mchakato unaoendelea. Hayaishi na hutofautiana kati ya mtu na mtu na kati utamaduni mmoja na mwingine. Kuna wakati yanaudhi, ni jambo kubwa kuelewa na kukubali mila na desturi za utamaduni wa wenyeji. Hii huambatana na kuutambua na kuuliza kuhusu utamaduni na utambulisho wako, jambo ambalo la manufaa zaidi ni kunufaika na kubadilishana kwa tamaduni. Mwisho wake mara nyingi husababisha mabadiliko ya mtu binafsi na wakati mwingine katika mazingira. Mchakato wa mabadiliko yako binafsi yanaweza kuhitaji uchunguzi sit tu wa tofauti katika utamaduni wako mpya bali pia maadili yako ya kitamaduni na mazoea. Kila hatua katika mchakato wa mabadiliko ya tamaduni huonyesha "vidokezo" au ishara za nje na ndani zinazowakilisha aina fulani ya tabia.



Kipindi cha Fungate

Awali, huenda ukatoa kipaumbele na kusiona na kila kitu kipya. Unaweza kufurahia kuwepo katika utamaduni mpya.

⁵ http://en.wikipedia.org/wiki/Culture_shock

Mshtuko katika Utamaduni

Mshtuko wa utamaduni hujitokeza mara unapoanza kujiingiza katika mambo ya utamaduni - kujizoeza malazi, njia za usafiri, chakula, lugha na watu. Mtu huchoka kadiri anavyofululiza kujaribu kujichanganya na kutumia lugha nyingine. Unaweza kuhisi kwamba huridhiki na ile hali hivyo kuanza kukosa uvumilivu, kuhuzunika, kukasirika, au kuzembea. Unaweza hata kushangaa ni kwa nini uliamua kwenda ugenini. Hata hivyo, hizi ni ishara nzuri! Kwani zinaonyesha si kwamba wewe unajaribu kupata mambo juu juu tu katika utamaduni mpya, lakini ukweli ni kwamba unajichanganya hasa kwa karibu zaidi.

Mabadiliko ya Awali

Katika kipindi hiki, kila kitu kama vile malazi na kwenda shule si matatizo makubwa kwako tena. Unajisikia huru kuonyesha hisia zako na kutoa maoni yako kupitia lugha ya wenyeji. Unaweza pia kuhisi hali mpya ya furaha na uchangamfu katika hatua hii.

Kutengwa Kiakili

Baada ya kipindi cha mabadiliko ya awali unaweza kuhisi hali ya mshtuko katika utamaduni inajirudiarudia, hii ni kutokana na hali ya kuwa mbali na familia na marafiki kwa kipindi kirefu na unaweza kujihisi upweke au ugonjwa wa kuwa mbali na nyumbani. Unaweza kuogopa kujieleza na kupendelea zaidi lugha ya taifa lako. Kukata tamaa na wakati mwingine kutojiamini hujitokeza, na ni katika hatua hii baadhi ya watu kuamua kurudi nyumbani.

Kukubalika na Kujichanganya

Katika hatua hii, utaweza kuanzisha mazoea (kwa mfano, kazi, shule, maisha ya kijamii) na kuanza kuzoea tabia, desturi, mila, vyakula, lugha, watu na nchi jinsi ilivyo.

Furaha ya Kurudi, Mshtuko wa Kurudia ile hali na Kujichanganya tena

Wakati mwingine kurudia mshtuko inaweza kuwa ngumu zaidi kuliko mshtuko wa utamaduni kwa sababu hatutarajii. Uwe tayari kukabiliana na mchakato wa marekebicho kama uzoefu ule ule ulioupata ugenini wakati unajaribu kujizoea utamaduni wa nyumbani ukiwa na familia na marafiki

Chanzo cha picha na maelezo: www.isc.sdsu.edu/study_abroad/accepted-culture-shock.html

Sababu za Ubaguzi na Ukandamizaji

“Ubaguzi ni tuhuma za chuki zisizo thabiti dhidi ya watu wa jamii nyigine. Ubaguzi unaweza kutokana na jinsi jamii moja inavyoitafsiri jamii nyingine kijuu juu na tafsiri hiyo ni makisio tu yanayooanishwa na sifa walizonazo wanajamii wa kikundi hicho kingine. Ubaguzi wakati mwingine huundwa kwa ajili ya kuoanisha mambo ambayo ama hayana maelezo ya uhakika au potofu au ya kufikirika. Ubaguzi unaweza kuwa na mtazamo mzuri au mbaya. Mara nyingi hujumuisha kikundi chote kwa jumla kutokana na uelewa mdogo kuhusu kikundi hicho alionao mtu anayekitungia ubaguzi huo. Watu wanaweza kubaguliwa kikabila, kidini, jinsia, umri au wingi wa sifa fulani walizonazo wanajamii wa kikundi hicho kingine 6.

*“Neno **Ukandamizaji** linahusu uamuzi wa haraka: ikimaanisha kutoa hukumu juu ya mambo kabla ya kuelewa kiini halisi cha tukio. Kwa kawaida neno hili linatumika katika kuelezea hali zenye utata kama vile 'ubaguzi wa rangi'. Awali lilitumika kumhukumu mtu kutokana na rangi, dini, n.k. kabla ya kupata maelezo sahihi yanayohusu jambo lenyewe; baadaye lilianza kutumika kama hisia yoyote ya kikatili kuhusu mtu iliyohusishwa na ubaguzi au hukumu zinazotolewa bila hata kumfahamu vizuri mtu. Hatimaye neno hili lilitafsiriwa kama kama namna ya ukandamizaji katika sehemu zenye ubaguzi. Maana ya neno hili kwa sasa imekuwa “msimamo wenye kupinga uamuzi wowote wa busara”. Rangi ya mtu, jinsia, kabila, umri na dini ni mambo ambayo katika historia yametolewa mifano ya tabia za ukandamizaji⁷*

Jinsi ya Kutofautisha

Kuna wakati maneno haya ukandamizaji na ubaguzi yanachanganya. Ukandamizaji ni mitazamo au tabia za jumla dhidi ya mtindo fulani wa maisha au aina ya watu.

Ubaguzi ni mitazamo ya dharau ya jumla kulingana na hali iliyopo. Hii hurahisha.

⁶ <http://en.wikipedia.org/wiki/Stereotype>

⁷ <http://en.wikipedia.org/wiki/Prejudice>

“Ukandamizaji na Jinsi unavyotumika kurahisisha Utoaji wa Maamuzi”

Katika maana ya kitaaluma, ubaguzi ni hukumu zinazotolewa kulingana na namna unavyomuelewa mtu au jamii yake. Ni chombo cha kitaaluma kinachofanikisha utoaji wa maamuzi ya haraka katika mazingira yenye mabadiliko ya ghafla. Kwa hiyo kinaweza kuwa cha manufaa kwa wale wanaojaribu kukabiliana na msukumo wa mabadiliko ya ukisasa. Wachache kati yetu tunaona tumemaliza siku iwapo tumeweza kutolea maamuzi kila jambo linalotukabili tukiwa kazini utafikiri hatujawahi kukabiliana na matatizo kama hayo.

Kwa bahati nzuri, watu wanaweza kupunguza suluba hiyo kwa kulinganisha na mambo ambayo yameshatokea siku za nyuma kwa sababu binadamu wamejaliwa akili na uelewa unaowawezesha kuweka kumbukumbu ya matukio ya siku za nyuma na kuweza kuyapanga na kujifunza kutokana nayo. Maoni mengi tunayoyapata, ama kutokana na uzoefu au kutoka kwa wenzetu au kutoka uzoefu wa wengi katika jamii, huitwa ukandamizaji. Haya ni maoni ya jumla yanayokubaliana au kupinga kitu fulani. Yanapooanishwa na uchunguzi halisi na uchambuzi wa busara, maoni hayo huonekana tu kuwa ni uzoefu. Uzoefu ni mwongozo ambao haukufanyiwa utafiti wa maisha ya kila siku, ambayo huwakilisha maamuzi yanayokaribiana na ukweli na huweza kutumiwa kufanyia maamuzi katika mazingira mapya ambayo kimsingi yapo sambamba na uzoefu wa siku za nyuma. Kwa ufupi, uzoefu umegundua kwamba watu wa aina moja ya kazi, iwe ya kitaifa, kijamii, kidini au kabila fulani huwa na tabia ya kufanya maamuzi yanayofanana katika mazingira yanayofanana na hivyo kuna uwezekano kwamba hata wenzao wengine walio katika kundi hilo wataishi kwa mtindo unaofanana na huo.

Uzoefu unatuonya kwamba ni muhimu kubuni njia za utendaji kazi zilizo sahihi zaidi. Kinadharia mtu mwenye busara na mwenye muda wa kutosha huweza kufikiria namna mpya ya kukabiliana na hali, lakini ni tofauti kwani watu wengi hujikuta kila mara katika hali ya kukosa muda au mwanya wa kutosha wa kufanya maamuzi yaliyo sahihi na hivyo hukimbilia uzoefu wa siku za nyuma ili waweze kuamua nini cha kufanya.

Kuwapokea waajiriwa wapya hutegemea zaidi uzoefu wa siku za nyuma, na jumla ya uzoefu wa mambo yaliyomo katika siku za nyuma, na hiki si kitu kingine bali ni kile kile ambacho hulaaniwa sana lakini ni muhimu yaani ‘ubaguzi’, upendeleo au vinginevyo. Mtu anaweza kubaguliwa kwa ajili ya kupenda au kupinga kitu fulani. Huu ni ‘ubaguzi’ wa kisomi’, njia fupi ya kufanya maamuzi inalenga zaidi uzoefu uliopita, kitu ambacho mtu ambaye ana shughuli nyingi za kufanya hawezi kuacha ili siku iishe.”

Kutoka: “Sura Mbili za Ubaguzi”, Alan McGregor

Mabadiliko ya Kitamaduni na Mapungufu yake

*“Mabadiliko ya kitamaduni yanahitaji uwe **mwepesi wa kushika mambo** na si kujitesa”*

Ili kuonyesha kuwa unaheshimu utamaduni wa wengine, ni muhimu **kujibadili kitamaduni kwa kukubaliana na baadhi ya kanuni za mahusiano ya kijamii**. Hii inamaanisha mavazi, namna ya kuongea na jinsi ya kusalimiana. Kwa mfano: kama wewe ni muislamu, ni lazima ule chakula au kutoa kitu kwa kutumia mkono wa kulia mkono mwingine huhesabiwa kuwa ni mchafu.

Hivyo ni muhimu uwe na uelewa wa baadhi ya tabia za kitamaduni ili kuepuka kuonekana mjeuri bila kujijua.

Haya mabadiliko ya juu juu ni rahisi iwapo hayana madhara kwa utamaduni wako mwenyewe. Kwa mfano: wanawake wengi wa nchi za magharibi hawavai hijab ya kiislamu kwa sababu inapingana na baadhi ya mambo ya msingi katika tamaduni zao.

Swali ni kwamba: Ni kiwango gani kinahitajika katika kuheshimu mabadiliko ya kitamaduni na nini ukomo unaohitajika katika kuendeleza maoni ya tamaduni zetu wenyewe?

Maoni yako, ambayo hutokana na asili ya utamaduni wako, huanzia pale maadili na kanuni za msingi za utamaduni wako ni tofauti au zinapingana na zile za utamaduni mwingine.

Kila mtu anatakiwa kuelewa yeye mwenyewe, ni kiasi gani anaweza kukubaliana na mabadiliko ya utamaduni mwingine na ni maeneo yapi yaliyomo katika utamaduni wake anatakiwa kuyaendeleza ili asiukane utambulisho wake.

Zana zinazotumika katika Mawasiliano ya Tamaduni na Ushirikiano

Mawasiliano katika tamaduni huweza kuwa pana na lenye ubunifu lakini mara kwa mara kwa ajili kutokuwa na uwezo wa kuwaelewa watu vizuri huweza kuwa kikwazo. Kujenga uwezo wa kuelewa tamaduni za watu wengine, namna wanavyowasiliana na tabia zao inaweza kudumisha ushirikiano na kuleta mafanikio katika mazingira yenye muingiliano wa tamaduni.

1. **Kuwa na Subira:** Kufanya kazi kwenye mazingira yenye muingiliano wa tamaduni linaweza kuwa ni jambo linalochanganya. Mambo yanaweza yasifanyike wakati unaotarajiwa, mawasiliano yanaweza kuwa yenye kuchosha na tabia zinaweza kuwa si sahihi. Kuwa na subira na kuwavumilia wengine husaidia kusonga mbele na kuepuka kujirudia kwa mambo kama hayo siku zijazo.
2. **Tunga Sheria:** Iwapo unafanya kazi na kikundi cha kweli chenye muingiliano wa tamaduni itabidi mtazame siku za nyuma na kutunga sheria za msingi yaani mbinu gani zitumike kukabiliana na mambo kama kujali muda (kuwahi), mikutano, mawasiliano, barua pepe, kutoelewana, n.k. Ni jambo la muhimu mara zote kujaribu kutunga sheria za kikundi kuliko kusubiri zitungwe kwa niaba yenu.
3. **Uliza Maswali:** Kama huelewi kitu au unataka kujua ni kwanini mtu ana tabia fulani, jambo rahisi ni kuuliza. Kuuliza maswali kutakuzuia kukisia, na itafanya unaowauliza maswali kutambua kuwa huwaelewi na itasaidia kuwa na akiba ya uelewa wa muingiliano wa tamaduni.
4. **Heshima:** Msingi wa mawasiliano katika tamaduni ni kuheshimiana. Ukionyesha heshima utaheshimiwa na itasaidia kutengeneza mahusiano yenye uwazi na mafanikio.
5. **Ucheshi:** Katika mazingira yenye muingiliano wa tamaduni utani wa mtu unaweza kuwa tusi kwa mwingine. Unatakiwa kuwa makini juu ya tofauti zilizopo katika namna ya ucheshi, kukubalika kwa utani na vitu kama hivyo katika sehemu za kazi.
6. **Daima kuwa Mwangalifu:** njia rahisi ya kupunguza athari mbaya zinatokana na mawasiliano katika tamaduni ni kuhakikisha unakuwa mwangalifu. Kama ni katika kukubaliana jambo au unatoa maelekezo, tumia muda kidogo kuhakikisha kwamba wote wanaohusika “mko pamoja”, hii itaokoa muda ambao utatumia baadaye kuiangalia kazi mstari kwa mstari.

7. **Kuwa Muwazi:** Wakati unakabiliwa na matukio ya muingiliano wa tamaduni tengeneza mazingira yatakayo epusha lawama na migogoro. Kukaa muwazi, yachambue maeneo yenye matatizo na fanya kazi kama kikundi ili mtengeneze mikakati na suluhisho la matatizo ili hakikisha kamwe hayarudiwi tena.
8. **Tafakari:** Jaribu kujitazama jinsi wenzako wanavyokuona na jaribu kuelewa ni kwanini wanaipinga tabia yako kwa namna wanavyofanya. Chukua muda kuelewa namna unavyowasiliana na wenzio, unavyoongoza na mbinu za uhamasishaji unazotumia ili uweze kuelewa ni jinsi gani unaweza kujirekebisha mwenyewe.
9. **Jifunze kwa Makini:** Ni kitu unafikiri wenzio wanaweza kujifunza kutoka katika utamaduni wako kuhusiana na kazi, shirika, mawasiliano, masomo fulani, n.k.? Jaribu kuwaelezea maoni yako ili uone kama watapenda kufuata mapendekezo yako. Jambo la muhimu zaidi: Jiulize kama kuna maeneo ya utamaduni mwingine yatakunufaisha katika mikakati yako pia!

Kurasa za Nyongeza

Makala ya 1: Tunamaanisha nini tunapozungumzia Utamaduni?

Jinsi inavyoelezwa na Taasisi ya Roshan (Ukuzaji wa uelewa kuhusu muingiliano wa tamaduni)

(<http://www.roshan-institute.org/templates/System/details.asp?id=39783&PID=474552>)

Culture is a definition highly misunderstood and misused, thus the need for an explanation:

Utamaduni huashiria namna mbalimbali zifuatazo za maisha na si vinginevyo:

sophisticate

Lugha: *taasisi/chombo cha zamani zaidi chenye ugumu fulani kinachotumiwa na binadamu katika kujieleza*

Sanaa na Sayansi: *njia za kisasa zaidi zinazotumiwa na binadamu katika kujieleza.*

Fikra: *namna ambavyo watu huitambua, hutafsiri na kuelewa dunia inayowazunguka.*

Mambo ya Kiroho: *ni mfumo wenye thamani ambao umekuwa ukirithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine kwa ajili ya kulinda usalama wa ndani wa binadamu, ambao huelezwa kupitia lugha na matendo.*

Shughuli za kijamii: *shughuli za pamoja za ndani ya kikundi cha kitamaduni zinazotumika kuonyesha aina mbalimbali za matukio katika sherehe na maadhimisho ya maisha.*

Mahusiano: *masuala ya kijamii yanayohusu mawasiliano ya binadamu, ikiwa ni pamoja kupeana na kujichanganya kijamii, majadiliano, itifaki na mikataba.*

Mambo yote hayo kwa pamoja ndio hutoa maana ya utamaduni.

Baadhi ya Fikra zinazohusu Utamaduni kama zilivyo-elezewa na Mshairi wa Kimarekani anayeitwa T.S. Eliot:

“Kama tukilitazama suala la utamaduni kwa kina, tutaona kwamba watu hawahitaji chakula cha kutosha tu bali huhitaji vyakula maalum [...] vilivyo sahihi. Utamaduni unaweza kuelezewa kirahisi kama kitu kinachofanya maisha yawe yenye thamani”.

“Kama mnataka kudumisha utamaduni, watu hawatakiwi wawe wameungana sana au wametengana kabisa”.

“Hakuna utamaduni unaoweza kujitokeza au kutengenezwa bila kuhusishwa na dini”.

“Si kwamba jamii isiyo na matabaka, au jamii iliyojengeka katika misingi isiyovunjika, ndio itahesabika kuwa ni nzuri, kila kikundi kinatakiwa mara kwa mara kiwe na kuleta mambo mapya na kujirekebisha; haya makundi, pamoja na kutakiwa yawe tofauti, yanatakiwa yaweze kujichangaya kirahisi na yanatikiwa yashirikiane katika tamaduni ili wawe na vitu vya pamoja vitakavyowafanya wawe wamoja, na ya msingi yanayohusu matabaka zaidi ya kikundi na kikundi kingine”.

“Mwisho, mtu historia yake huangalia zaidi mchango wake katika kukuza utamaduni wa watu wengine na pia huangalia mchango katika utamaduni utakaojitokeza baada ya hapo”.

Makala ya 2: Maana ya Utamaduni kama ilivyofafanuliwa na Kitengo cha Anthropolojia ya Utamaduni cha Chuo Kikuu cha Manitoba

Utamaduni: Mfumo wa pamoja wa imani, maadili, desturi, tabia, na kazi za sanaa ambazo wanajamii hutmia katika kukabiliana na dunia na kushirikiana kati ya mtu na mtu, na ambao hurithishwa kutoka kizazi hadi kwa njia ya mafunzo (p7).

Huu ni ufafanuzi tata ambao umejengwa katika mambo manne muhimu yafuatayo kama yanavyotiliwa mkazo katika nadharia za kitamaduni:

- (i) Miundo yenye mifano
- (ii) Mfumo wenye vielelezo
- (iii) Urithishaji wa mafunzo
- (iv) Msingi wa jamii

Jambo ka Kutilia Mkazo Na 1: Miundo yenye mifano

Jambo la msingi katika utamaduni ni wasifu wake. Wasifu hujionyesha kwa namna nyingi kuanzia mavazi, kazi za sanaa, vitendea kazi, majengo, inavyojali wakati/muda, ushirikiano wa kifamilia, mabadiliko ya uchumi, adhabu za kisheria na imani. Mambo haya mbalimbali yenye utata hufanana katika jambo moja; nalo ni kwamba huwa ni vielelezo vyenye kuleta maana.

Kielelezo kwa maana rahisi ni alama zinazowakilisha kitu kingine, mara nyingi ni hali halisi ya dunia. Matumizi ya maneno katika lugha ni mfano halisi. Maneno hutumika kuelezea fikra za watu na mataifa. Maneno kama vielelezo hutumika katika namna mbalimbali tofauti na vitu vinavyowakilishwa na yana sifa maalum. Sifa moja kuu ni kwamba hayahusiani na vitu vinavyowakilishwa na hivyo hayafanani. Tunaweza kumtaja mnyama mwenye maumbile ya kushangaza kama vile “domo kama la farasi”, masikio makubwa, mdomo umechongoka, kwa kutumia sauti zenye mpangilio tofauti kama vile pachyderm au osono. Jambo jingine la kuu katika vielelezo ni uwakilishi, yaani, maneno huweza kutumika badala ya vitu vinavyowakilishwa wakati wowote au mahali popote. Hivyo ninaweza kuzungumzia tembo na si lazima niwaagize tembo hao kutoka Afrika. Sifa hii inatuleta katika kipengele kikuu cha tatu, ambacho ni sanifu. Kwa sababu yametengenishwa na vikwazo vilivyomo katika vitu halisi, unaweza kutumia ujanja ukayabadili na yakaleta mpangilio mwingine. Kwa hiyo, tunaweza kutumia neon tembo kumaanisha vitu vyenye ukubwa ambao haujaozoeleka, mifano ya aina za tembo, ni wazee wa jadi tembo, tembo wanaoruka na miungu tembo.

Wakati maneno huleta mifano rahisi, vitu vya msingi katika tamaduni zote kwa mfano mavazi huonyesha vielelezo vya mifano halisi. Kazi za sanaa na tafrija ni maana ya wazi ya vielelezo halisi na huandaliwa kwa makusudi ili

kuwakilisha. Vitendea kazi na teknolojia ni vielelezo vyenye uhalisia kidogo, bali pia huwakilisha. Hutengeneza kutokana na mipango ya wastani ili kufikia malengo yanayotajwa kwa namna tofauti. Teknolojia pia hutupatia uwezo wa kubadili vielelezo halisi vya dunia na kuvibadili kuwa tembo na vifaru vya kweli vya vibonyezo vya kinanda.

Jambo ka Kutilia Mkazo Na 2: Mfumo wenye vielelezo

Vielelezo kama vitu vya msingi vinavyotumika katika utamaduni, hutoa maana inayohusishwa na vielelezo vingine katika muktadha mpana wa mfumo wa uelewa. Hivyo, ili kuweza kutafsiri kielelezo, wanaanthropolojia hulazimika kuchunguza uhusiano uliopo na misingi ya pamoja inayounganisha vielelezo hivyo katika kutengeneza mifumo mikubwa ya jamii nzima.

Tukichukua mfano wa kundi la Dani (jina la kabila) ambalo Heider amelitambua kama “jamii ya kivita”. Tutatumia vita vya Dani katika mifano mbalimbali ili tuweze kuelewa chanzo chake na athari zake. Zoezi la kwamza ambalo mwanaanthropolojia anatakiwa afanye ni kuelewa maana ya vita na ni vizuri pia ailinganishe na masuala mengine ya utamaduni wa kabila la Dani katika maana yao halisi. Katika kufanya hivyo inabidi tuachane na maana na misemo yetu kuhusu vita ambayo ni jinsi dola ya taifa moja inavyoelezea jinsi inavyogombea mali za asili adimu au athari za ukatili wa binadamu au ucheleweshaji wa kutokomeza kwa tabia ya kujamiiana katika umri mdogo.

Kitu cha kwanza kuelewa katika kabila la Dani ni kwamba katika lugha yao wana maneno mawili yanayohusu mapambano yanayohusisha silaha kubwa: yaani *wim and um'aim*. Heider anayatofautisha maneno haya mawili kama vile ni hatua mbili za kivita, ingawaje kwa kutumia njia hii ya tafsiri inaficha ukweli kwamba kila moja ina mfumo tofauti kimaana na kitabia.

‘Wim’ ni neno linalowakilisha utamaduni wa kivita unaofanywa kati ya wapiganaji wa mfumo tofauti ya kijamii au tawala lakini zinazofungamana. Wapiganaji wote hufungamana kwa kushirikiana katika tamaduni, lugha, imani na uelewa kuhusu ni kwanini na namna gani vita inatakiwa kuendeshwa. Ukatili kati ya pande hizi zinazofungamana huchukua sura ya uvamizi au vita rasmi; au utekaji nyara. Mpiganaji mmoja anapouwawa uvamizi huu au vita hii husimamishwa mara moja. Tukio lolote la kutisha likitokea hasa la mauaji, kundi ambalo mpiganaji wake ameuwawa huweka msiba wakati na huo huo kundi lililosababisha kifo hicho husheherekea (kundi lenye msiba huthibitsha kuhusu kifo cha mwanakikundi wao aliyeuwawa na kuwasilisha taarifa hizo ikiwemo jina la aliyeuwawa kwa kikundi kilichosababisha kifo hicho). Kikomo cha kuzuia ukatili kilichorithiwa katika mfumo huu wa kivita, ambapo mtu mmoja tu huuwawa wakati wa mapambano, husaidia kupunguza idadi ya vifo na uwiano wa kati ya maadui ambapo hakuna rasilimali zaidi zinazoharibika. Mfumo huu pia hudumisha mtindo kwamba wanaume wanalo jukumu la kulinda, kupambana na kusheherekea.

Kikomo cha ukatili kilichorithiwa katika mfumo huu, ambapo ni mtu mmoja tu huuwawa kwenye mapambano, husaidia kupunguza kiwango cha mauaji na uwiano wa kati ya wapinzani ambapo hakuna himaya iliyomzidi mwenzake. Na pia huichukulia vita au mapambano kama hali fulani isiyo na mwisho ambayo huwafanya wanaume kujiona wana wajibu wa kulinda, kupigana na kufanya sherehe.

Jambo muhimu na la kuzingatia ambalo unaweza kuona ni tofauti na tamaduni zetu, hasa za kivita, ni kwamba mfumo wa kivita wa Kundi la Dani umechanganya elementi zinazojitokeza katika tamaduni za magharibi kwenye mfumo tofauti tatanishi ambao huusishwa na taasisi nyingine za Kundi la Dani ambazo zina mifumo ya tamaduni tofauti tofauti ikilinganishwa na mfumo wenye utamaduni mmoja. Kundi la Dani hutoa maana nzuri ya mfumo wao pale wanapoelezea vita kwa kulinganisha na imani yao juu ya mizimu. Wao huamimi kwamba mtu anapouwawa, mzimu wa kundi lililopoteza mtu wao litataka kulipiza kisasi na litawasumbua mpaka adui aliyehusika na mauaji atakapouwawa. Baada ya hapo sherehe zitafanywa ili kuituliza mizimu ya pande hizi mbili zinazohusika. Hali hii hujirudiarudia kwa sababu kila mara kifo kitakapokuwa kinatokea maana yake shughuli hiyo lazima ifanywe kuikabili hiyo nakama. Umuhimu wa dini; na urasimishaji na usheherekeaji wa ukatili, umemfanya Heider kuuita mfumo huu kuwa ni ‘mafunzo ya awali’ ya kivita.

Katika mwongozo huu tutarejea tena kujifunza namna ‘mafunzo ya awali’ na “aina” nyigine ya ‘kivita ya secular’ au kama inavyojulikana katika sehemu nyingine ‘um'aim’ vinavyotofautiana. Kwa sasa tunaweza kuhitimisha kwamba sifa na vielelezo vya utamaduni ni vyema vikieleweka tangu mwanzo kwa mantiki ya kuuelewa utamaduni na namna ya kushirikiana katika utamaduni kwa kuzingatia mandhari au kiini thabiti na kanuni zake. Mtazamo huu unaitwa ‘holism’ ambalo humaanisha kwamba huwezi kuzielewa sifa za utamaduni mmoja katika hali ya utengano.

Jambo ka Kutilia Mkazo Na 3: Urithishaji wa Mafunzo

Sifa na mifumo ya jumla ya tamaduni ambayo hujumuisha lugha, teknolojia, taasisi, sifa na imani vimekuwa vikirithishwa na kudumishwa kutoka kizazi hadi kizazi kupitia njia ya mafunzo inayoitwa ‘enculturation’.

Vivyo hivyo, uwezo na akili ni rasilimali za maana kwa jamii zote za binadamu na zimefanikiwa kuchukua nafasi ya urithishaji wa kibaiolojia ambao msingi wake ulikuwa kwa njia ya maumbile wenye silika kubwa kwa wanyama wengine. Hata hivyo, uhusiano muhimu kati ya biolojia na utamaduni lazima kwanza utambulike.

Baiolojia ya binadamu imeathiri maendeleo ya utamaduni tangu mafunzo kwa vitendo yalipoanza kutegemea muundo wa ubongo na milinganisho mingine ya kurithi ya kimaumbile kama vile miundo wa sauti ambao huweza kutengeneza hotuba au mwongozo unaoweza kutengeneza vifaa. Hii dhana ya baiolojia imekuwa mhimili unaojumuisha uwezo wa utamaduni kati ya binadamu wote na ndio hutoa maelezo juu ya sifa/vipengele vya jumla kuhusiana na mambo mbalimbali kama vile uwezo wa kujifunza lugha. Hata hivyo, vigezo vinavyotumika katika baiolojia haviwezi kubahinisha tabia/sifa za kitamaduni kama vile uwezo wa kuongea Kifaransa, Kiingereza au Kidani. Watoto wote kabla hawajazaliwa hupitia mpango ulio katika hatua maalum mbalimbali ambazo huwarithisha uwezo wa kujifunza na kuelewa lugha, lakini hushika lugha fulani maalum tena kwa maelekezo. Kwa hiyo baiolojia huweza kutambua uwezo wetu wa kitamaduni kwa ujumla na inahusika na kutoa maelezo ya kwa nini tunaonekana jinsi tulivyo, kwa mfano sifa zinazojitokeza katika kila tamaduni zilizomo duniani. Hata hivyo, tofauti za kitamaduni kati ya watu mbalimbali zinatokana na mila za kujifunza na si kwa sababu ya asili au maumbile ya mtu.

Kubadilika kwa urithishaji wa maumbile ya tabia kwa kujifunza wakati wa ukuaji wa binadamu imeleta madhara ya wazi juu ya urithishaji wa kibaiolojia. Kwa sasa tunajiozea mazingira kwa kutumia mbinu za kitamaduni kuliko kutumia urithi wa urithishaji wa kimaumbile. Vivyo hivyo, makundi ya binadamu yameenea kila mahali duniani na kuhimili tofauti kubwa sana zilizopo katika hali ya hewa na vyakula bila kuzulika na tofauti za kianatomia. Matokeo yake imekuwa kwamba, aina mbalimbali za kimaumbile kati ya watu, ambazo zimejitengeneza kwa zaidi ya mamilioni ya miaka katika maelfu ya mazingira ya aina mbalimbali, ni kitu kinachoshangaza hasa. Tofauti za kitamaduni hata hivyo, zimekuwa kubwa na zisizo na mwisho na zimetengeneza jambo lenye kuvutia linalohitaji kufanyiwa uchunguzi wa kianthropolojia.

Jambo ka Kutilia Mkazo Na 4: Kuhusishwa na Jamii

Utamaduni hujionyesha tu katika mfumo wa tabia ya mtu binafsi lakini pia huweza kujionyesha katika matendo ya mtu mmoja mmoja lakini badala yake umekuwa ukihusishwa zaidi na jamii watu hao wanakotokea. Vivyo hivyo, wananthropolojia hawatilii mkazo mkubwa katika umuhimu wa wajibu wa mtu mmoja mmoja na ubunifu badala yake mkazo umekuwa ukiwekwa katika vitu vya kawaida vya pamoja vinavyoashiria na kuitambulisha hiyo jamii. Hali hii imetoa kielelezo cha kisasa ni kwa nini kuna umuhimu wa kuwepo haki na matendo ya mtu mmoja mmoja. Hata hivyo, kuna vitu vichache vinavyoonyesha kwamba jamii huelezea zaidi na kuathiri tabia za watu kwa namna nyingi ambazo hazitambuliki. Tunaweza kuelewa vipengele vya kijamii katika utamaduni iwapo tutatambua kwamba kiini cha utambulisho wa binadamu ni mawasiliano ambayo huwa na mambo muhimu ya kuzingatia ili kuweza kuelewa makubaliano yaliyopo.

Sisi kwa makusudi kabisa tunapitia mivutano ya kijamii ambayo kuwa katika mfumo wa vikwazo vya kisheria iliyo katika misingi ya kitamaduni, lakini kanuni na mila za kijamii hutuzuia kutenda yasiyofaa kwa kiasi kikubwa. Hakuna sheria inayonilazimisha kwamba lazima niwasiliane na wewe kwa kutumia lugha ya Kiingereza, lakini inanilazimu kufanya hivyo kutokana na ukweli kwamba tuna uhusiano wa kijamii ambao unanifundisha kuwatambua wenzangu. Katika hali isiyo ya kawaida, mimi au wewe tunaweza kutumia lugha nyingine na kuhisi kwamba mwenzangu atajifunza au ataweka mtu wa kumtafsiria. Hata hivyo, sitakiwi kutumia ubunifu wangu kuanzisha lugha yangu binafsi.

Mfano wa pili unahusu uchaguzi wa mavazi. Hapa darasani, mimi sifundishi ni vazi bora linalotakiwa, isipokuwa ninafundisha darasa namna ya kuvaa mbele ya watu na pia huwa mnakumbwa na tatizo la nguo gani utavaa unapokwenda darasani. Ni kweli kwamba kuna sheria zinazotubana katika jinsi tunavyochagua nguo ya kuvaa, kwa mfano huwezi kutoka nje ukiwa uchi, lakini kuna miiko michache sana inayotubana pia. Watu wa zamani walijiwekea mipaka sahihi ya namna ya kuvaa. Inabidi tuvae majoho ya kitaaluma ili kuonyesha hadhi zetu. Baada ya muda, nguo zenye mtazamo wa kisomi zitakuwa hazitambuliki katika mitindo ya kisasa, na itabidi tuvae mavazi ya kibiashara yenye nakshi, ingawaje majoho bado yatahitajika katika kazi za kitaaluma.

Katika miaka ya 1960, maadili yaliyopingana na utawala wa kimabavu yalileta uvaaji wa suruali mpya zilizosanifiwa za 'jeans' na mashati ya kufanyia kazi. Kwa sasa tuna uhuru mkubwa wa kuchagua mitindo ya aina yoyote ya mavazi tunayopenda kuvaa, lakini bado ipo miiko madhubuti ya kitamaduni inayotuzuia. Nisingeweza kuja darasani nikiwa nimevaa nguo ya kuogea, hata kama ni kipindi cha joto ambapo kwa ukivaa hivyo unapata nafuu mwilini. Nikiwa mwanamume sikuruhusiwa kuvaa viatu vyenye mchuchumio mrefu na sketi fupi, bila kusababisha mtazamo usiotakiwa ambao ungenipunguzia ufanisi katika utendaji wangu wa kazi.

Maana na ukomo wa kanuni zinazohusishwa na jinsi ya uvaaji zinatatanisha na ziko katika mfumo mbalimbali katika tamaduni nyingine. Wanaume katika Milima ya Mayan na wanawake wa jamii ya Guatema wa San Antonio inawabidi wafuate sheria za uvaaji ambazo numtaka kila mtu katika kijiji avae nnguo ya aina moja. Tukifananisha na mavazi ya Magharibi, tutaona kwamba nguo za wanaume na wanawake wote wanavaa blauzi na vibwaya (yaani sketi wanazovaa kwa kuzungusha kiunoni) na hivyo tajikuta tunapata maswali kuhusu jinsia ya wanaume wa Hamayan.

Hata hivyo, ukiangalia kwa makini mchoro ulioonyeshwa hapo juu unaelezea kwamba wanaume na wanawake wa San Antonio huvaa kwa namna ambayo hutofautisha wazi wazi mavazi ya kike na kiume. Mavazi yao hutofautishwa kwa rangi ya viblauzi; wanaume huvaa rangi nyekundu na fulana zenye

mistari myeupe na mikono yenye rangi nyekundu; wakati wanawake huvaa kinyume kabisa cha wanaume. Pia, kutofautisha majukumu kijinsia, mifumo ya mavazi ya watu wa Milima ya Mayan pia hutambulisha mtu ni mwanachama wa jamii gani, kwa vile kila kijiji kimejipangia vazi tofauti ili kuepusha utata katika kutambua watu wake.

Wakati mkazo mkubwa umewekwa katika vya vigezo vya kijamii kuhusiana na tabia za mtu mmoja mmoja ambazo ni za msingi katika dhana ya utamaduni, wanaanthropolojia wamekuwa wakivuka mipaka yao kiasi cha kusahau kuhusu athari zitokanazo na tabia ya mtu mmoja mmoja kabisa. Kwa hiyo, watu wamekuwa wanaonekana kama wasanii katika michezo iliyoandikwa na kuongozwa na mhariri mwenye akili za ziada anayelitwa 'utamaduni' au 'jamii' (tabia hii imepewa jina la 'reification', mfumo unaotumika kuhusisha vitu asilia na misemo mbalimbali. Utamaduni na nguvu za kijamii hujitokeza wazi wazi tu katika tabia za mtu mmoja mmoja, ambao nao huathiriwa na aina mbalimbali za nguvu za asili, kama vile nguvu za kisaikolojia, matarajio ya mtu binafsi, na fikra za ubunifu. Mtazamo wa kiantropolojia juu ya dhana ya utamaduni hutupatia sehemu ndogo tu ya ukweli kuhusu binadamu na inabidi tuazime au tushirikishe taaluma nyingine ili kuweza kuelewa kwa ujumla kuhusu uzoefu wa binadamu.


Chanzo:

www.umanitoba.ca/faculties/arts/anthropology/courses/122/module1/culture.html

Makala ya 3: Mfano/Kielelezo cha Iceberg

Utamaduni unaweza kuelezwa kwa kutumia mfano au Kielelezo cha Iceberg. Kuna sehemu ndogo ya utamaduni wa kutoka nje ambayo kila mmoja anaweza kuiona. Hii inaonekana katika sehemu ya juu ya Kielelezo cha Iceberg. Lakini sehemu kubwa ya Kielelezo cha Iceberg imefunikwa na maji, haionekani. Vivyo na utamaduni sehemu kubwa imezibwa na mambo ambayo ni dhahiri, sehemu ya nje imejengwa juu ya kitu ambacho kiko ndani sana.

Kielelezo hiki pia kinaweza kutumika kuelezea migongano katika tamaduni. Hebu fikiria icebergs mbili zikiwa baharini. Ingawaje sehemu zinazoonekana hazigusani, sehemu zisizoonekana ambazo zimefichwa chini ya maji tayari zitakuwa zimeshagongana. Kwa hiyo kabla hata hatujawasiliana au kuonana, tamaduni zetu zinagongana!



Makala ya 4: Utamaduni wa Albatros - Uigaji

Majukumu

Wahusika katika mchezo husubiri nje wakati waigizaji wawili, “Waalbatros” wakiandaa chumba. Kuna viti viwili na bakuli lililojaa karanga.

Baadaye mhusika mmoja anaitwa aingie ndani.

Waalbatros husubiri ndani. Hawavai viatu.

Wakati wageni wanaingia, Waalbatros humuonyesha kwa sauti za kuzomea kwamba anatakiwa kuvua viatu. Iwapo mgeni hataelewa, Waalbatros wao wenyewe humvua viatu (mwanaume humvua mwanaume na mwanamke humvua mwanamke).

Watu wote hukizunguka chumba mara moja, mwanaume akiwa anaongoza. Baada ya hapo, mwanaume mmoja mgeni hukalishwa juu ya kiti kimojawapo, na mwanamke mmoja mgeni huambiwa apige magoti. Mara wahusika wote wanapokuwa wameingia ndani huku wakiwa wamevua viatu vyao, huketi na kupiga magoti chini, mwanaume mmoja Mhalbatros hukaa katika kiti kingine na mwanamke mmoja Mhalbatros huchota karanga. Kwanza, huweka karanga kiasi katika mdomo wa Mhalbatros mwanaume, zilizobaki huzila mwenyewe. Huchukua tena karanga kiasi na kuziweka mdomoni mwa mwanaume mgeni, zilizobaki humpelekea mwanamke mgeni ambaye yeye hujichukulia mwenyewe.

Baadaye, Mhalbatros mwanamke hupiga magoti chini. Kisha Mhalbatros mwanaume huweka mkono juu ya bega la mwanamke yule aliyepiga magoti ambaye huinama kuelekea ardhini. Baada ya hapo Waalbatros huwaonyesha wageni ishara kwamba nao wanatakiwa kufanya vivyo hivyo, Waalbatros huwazungusha katika chumba zaidi ya mara moja, mwanaume akiwa ametangulia mbele na baadaye wanaondoka.

Maelezo na Ufafanuzi juu ya Igizo

Hatua ya Kwanza: Elezea kilichotokea, ni kitu gani ulichoona (tumia kifaa cha kuning'niza cha kufundishia kiitwacho 'flip chart')

Hatua ya Pili: Ulijisikiaje, je mambo hayo yote yana maana gani? Toa ufafanuzi (tumia kifaa cha kuning'niza cha kufundishia kiitwacho 'flip chart')

Chimbuko/Chanzo

Utamaduni wa Waalbatros unafuata mfumo wa kijamii ambao wanawake ndio hutawala, na Waalbatros kuamini kwamba dunia ni (mwanamke) ambaye ni mungu. Miguu mikubwa huthaminiwa na kuonekana ya kupendeza kwa sababu inakusaidia kugusana kwa karibu zaidi na Mungu wa Kike Dunia, na muda wote unatakiwa kutokuuachia uhusiano huu. Viatu huonekana kama vinazuia mtiririko wa nguvu ziletwazo Mungu wa Kike katika dunia kupitia mwili wako, kwa hiyo Waalbatros huwapatia wageni wao heshima ya pekee kwa kuwavua viatu vyao.

Kwa vile mwanamke huzaa kiumbe chenye hai, sawa sawa na Mungu wa kike ambaye ndio dunia, hupewa hustahiki. Waanaume wanatakiwa kuwalinda kwa kutembea mbele yao ili kuwakinga na madhara. Pia wanawajibika kuonja vyakula vyote kabla wanawake hawajala ili wasije wakadhurika. Kwa vile vyakula vyote hutoka kwa Mungu wa Kike Dunia, huwa ni vitakatifu, wanawake tu ndio wanaruhusiwa kuvigusa kwa mikono yao. Zaidi ya hapo, wanawake tu ndio wanaruhusiwa kuketi chini kwenye sakafu ili waweze kugusana vizuri zaidi na Mungu wa Kike Dunia, wakati wanaume wanatakiwa kuketi juu ya viti, mbali na Mungu. Katika sherehe za kuabudu, hata hivyo, wanaume wanaruhusiwa kuweka mikono yao juu ya migongo ya wanawake. Wanawake huanama kuelekea ardhini ili wanaweze kunyonya/kufyonza nguvu zote zinazotoka kwa Mungu wa Kike Dunia, na kwa kupitia mwili wa mwanamke, huisafirisha nguvu ile kwenda kwa mwanamme ili apate sehemu ndogo ya nguvu ya dunia kupitia kwake.

Majadiliano: Ni sehemu gani ya ufafanuzi inatatanisha? Ni kwa nini? Kuna baadhi ya sheria/kanuni zinaweza kuwa na maana tofauti kabisa katika utamaduni mwingine.

Ni jinsi gani tunaweza kuepuka kutokuelewana?

1. Chunguza
2. Fikiria
3. Fafanua
4. Toa uamuzi

Makala ya 5: Utamaduni na Migongano

Jinsi Utamaduni Unavyofanya Kazi

Ingawaje kwa kiasi kikubwa chini ya uso wa dunia, utamaduni ni mjumuiiko wa mambo yanayohama hama, na yneye upana sana lakini una vyanzo ambavyo hutuongoza njia zipi tuzifuate na kutuzuia kuelekea sehemu nyinginezo. Kila mmoja wetu hutokea katika jamii zinazoamini tamaduni za aina mbalimbali zinazotupa miongozo ya kipi ni cha kawaida, kipi ni sahihi na kipi kinachotarajiwa. Wakati wengine wanaposhindwa kukidhi matarajio yetu, tuelewe kwamba matarajio ya tamaduni zetu ni tofauti. Tunapokoseana kati yetu na wengine, ni ushahidi wa kutosha juu ya hisia potofu tulizonazo juu ya wengine au kutotumia hekima katika kuwaelewa wengine, bila kukumbuka kwamba hekima pia ni utamaduni. Hivyo kitu ambacho ni kawaida kwa jamii moja kinaweza kuwa cha ajabu, kinyume au makosa kwa jamii nyingine.

Ujumbe wa utamaduni hurekebisha uelewano katika mahusiano na jinsi ya kukabiliana na migongano na maelewano vitu ambavyo havikosekani watu wawili au zaidi wanapokusanyika pamoja. Kuandika au kufanya kazi zinazohusu utamaduni zinatatanisha, lakini si vigumu. Ifuatayo ni baadhi ya matatizo yanayojitokeza unaposhughulikia undani wa migongano ya kitamaduni na mambo yanayojitokeza:

Utamaduni una matabaka mbalimbali; kile kinachoonekana kwa juu huenda kikawa kimeficha kitu tofauti kwa chini.

Kwa hiyo, mjumuisho wa utamaduni sio hadithi nzima, na hakuna namna nyingine ya kutengeneza mahusiano na kupeana uzoefu, ili kuwafahamu wengine kwa undani zaidi.

Utamaduni mara kwa mara huwa katika hali ya kutokuwa na uhakika juu ya nini kifanyike, jinsi hali zinavyobadilika, makundi ya kitamaduni hujibadili ili kuendana na shughuli maalum au hali fulani kwa kutumia njia ambazo mara nyingine hazitabiriki na zinahitaji kutumia maarifa makubwa.

Kwa hiyo, hakuna maelezo ya kina ambayo yanayoweza kuandaliwa juu ya kikundi fulani. Namna yoyote ya kutaka kukielewa kikundi ni lazima vigezo mbalimbali vitumike kama vile wakati, mazingira na tofauti za mtu mmoja mmoja.

Utamaduni unanyambulika; hivyo kujua kanuni za kiutamaduni za kikundi fulani hazikusaidii kubashiri tabia za mwanachama mmoja mmoja wa kundi hilo, ambaye anaweza kuwa haendani na kanuni kwa sababu zake binafsi au kimuktadha.

Kwa hiyo, taksonomia mbalimbali (kwa mfano, “Waitalia hufikiria namna hii”, au “Wabudha hupendelea hivi”) zina nafasi ndogo, na zinaweza kutukosesha kama tusipotumia uzoefu.

Utamaduni kwa kiasi kikubwa uko chini ya uso wa dunia, hivyo ili kuweza kumvutia mtu kwa utambulisho wetu au vitu vyenye kuleta maana, au wale tunaoamini kuwa ndio hao na tunaowajali; sio rahisi kuzifikia ishara hizi kwa vile ziko nje kabisa ya upeo wa uelewa wetu.

Kwa hiyo, ni muhimu tukitumia njia nyingi ya kujifunza kuhusu vigezo vya utamaduni vya wale wanaohusika katika migongano, hasa njia isiyokuwa ya moja kwa moja, ikiwemo hadithi, mafumbo, na mila.

Umuhimu wa mvuto na utambulisho katika utamaduni hutegemea mazingira. Wakati hali ya utambulisho katika utamaduni ni inatishiwa au haieleweki, inaweza kuwa muhimu zaidi kuliko utambulisho wa utamaduni nyingine, na mara nyingi haibadiliki, hivyo utambulisho finyu huwa na lengo la kibaguzi, ni wa makisio tu na mgogoro. Hii ni hali ya kawaida sana katika migogoro inayoleta hofu kubwa.

Kwa hiyo ni muhimu kwa watu walio katika migogoro kujenga mazoea ya ushirikiano ambayo yatawawezesha kila mmoja kumuelewa mwenzake kwa mapana zaidi, uzoefu ambao utapelekea kutambua mambo ambayo yanawatambulisha wote kwa pamoja na yale ambayo yanawatofautisha.

Kwa vile utamaduni uko karibu sana na utambulisho wetu (namna ile tunavyofikiri kwamba ndivyo tulivyo), na namna tunatoa maana ya mambo (nini ni cha maana kwetu na kwa namna gani), mara nyingi umekuwa kati ya sababu za migogoro. Utambuzi wa utamaduni umetufanya tutumie ‘Kanuni ya Platinum’ badala ya ‘Kanuni ya Dhahabu’. Badala ya msemo “watendee wengine kama vile ambavyo ungependa wakutendee” Sheria ya Platinum inashauri kuwa “watendee wengine kama vile ambavyo wangependu uwatendee”.

Utamaduni na Migogoro: Uhusiano wake

Tamaduni zimo katika kila mgogoro kwa sababu migogoro husababishwa na mahusiano ya binadamu. Tamaduni huathiri jinsi tunavyoita majina, tunavyopeana lawama na jinsi tunavyotengeneza migogoro. Iwapo migogoro kweli ipo nalo ni swali kitamaduni. Katika mahojiano yaliyofanyika nchini Canada, mzee mmoja wa makamu wa Kichina alijitokeza na kuonyesha kuwa hana uzoefu wa migogoro wa aina yoyote katika miaka 40 iliyopita. Miongoni mwa sababu alizotoa ni uamuzi wake wa kuitazama dunia kwa kutumia miwani ya amani zaidi ya migogoro, kama ambavyo alikuwa akishauriwa na mlezi wake. Tunapoamua kuipa majina baadhi ya miingiliano yetu kuwa ni

migogoro, na kuifafanua katika sehemu ndogo ndogo, ni mtazamo dhahiri wa nchi za Magharibi ambao huweza kutufumba tusione vipengele vingine vya mahusiano.

Utamaduni siku zote umekuwa ni chanzo cha migogoro, haijalishi iwapo ina jukumu kubwa au inaathiri taratibu au pole pole. Kwa mgogoro wowote unaotugusa inapohusika, pale tunapopata maana na kushikilia utambulisho wetu, ni lazima siku zote pana suala la utamaduni. Migogoro inayotuingiza katika hofu kubwa kama vile mgogoro kati wana wa Israel na Wapalestina au mgogoro wa India na Pakistan juu ya Kashmir si tu unahusu utawala, mipaka ya nchi na masuala ya uhuru; bali pia suala la kukubalika, uwakilishi, na legitimization za utambulisho tofauti na njia tofauti za maisha, uwepo, na namna kila mtu anavyotafsiri mambo.

Migogoro kati ya vijana wadogo na wazazi wao hutengenezwa na utamaduni wa kurithishwa toka kizazi hadi kizazi, na migogoro kati ya mume na mke au watu wanaoshirikiana husukumwa na utamaduni wa kijinsia. Katika mashirika, migogoro inayotokana na tofauti za kinidhamu katika tamaduni mbalimbali huleta mvutano kati ya wafanyakazi, hujenga mawasiliano yasiyo sahihi au yenye kupinda panda na vikwazo katika mahusiano. Utamaduni unaruhusu migogoro bila kujali chochote; wakati mwingine huweka msukumo mkali wenye nguvu, wakati mwingine kimya kimya, ni vigumu mno kuelezea namna unavyojitokeza mara nyingi watu hushangaa wameshaingia.

Utamaduni hauwezi kutenganishwa na mgogoro, ingawaje hauusababishi. Wakati tofauti zinapojitokeza katika familia, makampuni au jamii, utamaduni mara nyingi lazima uwepo, kuweka sawa mitazamo, hisia, tabia na matokeo.

Wakati vikundi vya utamaduni vinatokana na taifa au jamii ya walio wengi, uwezekano wa kuelewa ujumbe ulitolewa unakuwa ni mdogo. Utamaduni unaoshirikisha makundi makubwa mara nyingi inaonekana ni ya "asili, au "kawaida"; "namna mambo yanavyofanyika". Tunatambua athari za tamaduni ambazo ni tofauti na za kwetu, kwa kushiriki katika mienendo ambayo sisi huiita ya kigeni au ya ajabu.

Ingawa utamaduni unafungamanishwa na migogoro, lakini baadhi ya njia zinazotumika katika kutatua migogoro zinapunguza masuala ya kitamaduni na athari zake. Kwa vile utamaduni ni kama bonge la barafu, ambalo kwa kiasi kikubwa huwa limedidimia, ni muhimu ukitumika katika chambuzi na hatua tunazochukua kukabiliana na mambo. Mabonge ya barafu yasipotambuliwa ni hatari na yanaweza kuleta ugumu katika kufanya maamuzi hasa kama hatufahamu ukubwa wake na mahali yalipo. Tukiutambua utamaduni na kuleta maana katika migogoro inaweza kuwasaidia watu wa aina zote katika kufanya maamuzi yaliyokusudiwa na kupendekezwa.

Utamaduni na Migogoro: Mwitikio wake

Kutokana na umuhimu wa utamaduni katika migogoro, ni nini kifanyike ili kuweza kuikumbuka na kuitumia katika kuleta majibu ya mipango yetu? Tamaduni zinaweza kuwa kama watoto wenye matatizo ya kiakili: ambao huwezi kuwaelewa wala kutabiri. Kama tukikubali utamaduni uwe ni sehemu ya migogoro, tutajikuta tumenaswa katika utatanishi wake, tukiwa tumebanwa na miwani ya tamaduni zetu. Fasihi ya tamaduni ni chombo muhimu katika kutatua na kushughulikia matabaka na migogoro ya kitamaduni.

Fasihi ya utamaduni maana yake ni utambuzi wa tamaduni: asili yake, namna zinavyofanya kazi na njia zinavyounganishwa na mahusiano yetu wakati wa migogoro na wakati wa amani. Fasihi ya utamaduni ni utambuzi wa vigezo mbalimbali vinavyotumika katika utamaduni ambavyo hujumuisha:

- (i) Mawasiliano'
- (ii) Njia zinazotumika kuita majina, kutunga na kuifuga migogoro;
- (iii) Namna tunatengeneza maana; na
- (iv) Utambulisho na wajibu wetu.

Ufafanuzi wa vigezo hivi ni kama inavyoelezwa kwa undani hapa chini.

Mawasiliano ni hatua mbalimbali ambazo huanzia na jinsi tunavyohusiana na wengine. Kuna tofauti nyingi katika hatua hizi. Baadhi ya tofauti kubwa ni zile zinazohusiana na mgawanyiko wa mawasiliano; kati ya walio katika mazingira ya hali ya juu na wale walio katika mazingira ya hali ya chini, uainishaji uliobuniwa na Edward T. Hall.

Mawasiliano katika mazingira ya hali ya juu, sehemu kubwa ya ujumbe hujionyesha katika mazingira, badala ya kujieleza kwa matamshi. Mandhari, jinsi maneno yanavyotamkwa, na maelewano ya pamoja ni miongoni mwa vitu vinavyosaidia kuleta maana katika mawasiliano. Njia rasmi za mawasiliano na mila zilizosarifiwa, huelezea mawazo bila ya kutamka. Matukio na ishara zisizohitaji maelezo ni muhimu katika kuuelwa ujumbe. Mazingira yanategemewa sana katika kuwasilisha ujumbe mahali ambapo hakuna mawasiliano yanayotumia ishara au wakati mwingine huwa kama nyongeza. Mawasiliano katika mazingira ya hali ya juu, yanaweza kuokoa muonekano wa juu kwa sababu sio ya moja kwa moja kama ilivyo katika mazingira ya hali ya chini, lakini yanaweza kuongeza uwezekano wa kutowasiliana kwa sababu sehemu kubwa ya ujumbe uliokusudiwa hautamkwi.

Mawasiliano katika mazingira ya hali ya chini husisitiza ujumbe wa ana kwa ana kuliko kutegemea mazingira yajieleze. Tukianza hapa, mawasiliano kwa njia ya maandishi ni ya uhakika na yenye uhalisia, na sehemu ndogo tu huelezewa kwa kuashiria. Mawasiliano katika mazingira

ya hali ya chini huwa na tabia ya “kusema wanachomaanisha na kumaanisha wanachosema“. Mawasiliano katika mazingira ya hali ya chini yanaweza kusaidia kuzuia mifarakano, lakini yanaweza pia kusababisha migogoro kwa sababu ni ya kukabiliana zaidi kuliko ilivyo katika mawasiliano katika mazingira ya hali ya juu.

Kwa jinsi watu wanavyowasiliana, ndivyo wanavyozidi kuelewana kati ya wale walio katika mazingira ya hali ya juu na wale walio katika mazingira ya hali ya chini. Kulingana na uhusiano uliopo, mazingira na lengo la mawasiliano, wanaweza kuwa wawazi zaidi au wanaojieleza moja kwa moja. Katika uhusiano wa karibu, mawasiliano kwa njia ya hatimkato hutumika mara nyingi, ili kufanya mawasiliano yasiwe ya wazi kwa wageni ila yaeleweke wazi kabisa kwa wenyeji. Mkiwa na wageni, watu hao hao wanaweza kutumia mawasiliano ya hali ya chini.

Mawasiliano katika mazingira ya hali ya juu au ya chini hayasaidii kuelewa mikakati ya mtu mmoja mmoja, bali yanaweza kutumika kuelewa vikundi vya kitamaduni. Kwa ujumla, tamaduni za Magharibi huwa na tabia ya kuanzia katika hatua mpya za mazingira ya hali ya chini, wakati tamaduni za Mashariki na Kusini huwa na tabia ya kuanzia mawasiliano ya mazingira ya hali ya juu. Ndani ya makundi hayo makubwa, kuna tofauti kubwa sana ambazo ni nyingi pia. Wakati mawasiliano ya mazingira hali ya juu hujulikana zaidi, ni bora tukiyapa kipaumbele mawasiliano ya ishara yasiyo na matamshi na tabia za wengine ambao wanaweza kuelewa zaidi kanuni zinazoongoza mawasiliano. Mahali ambapo mawasiliano ya hali ya chini ni ya kawaida, uwazi unatarajiwa kuwepo.

Kuna njia nyingi ambazo zinafanya mawasiliano yatofautiane kati ya utamaduni moja na mwingine. Tofauti hizo ni mawasiliano ya hali ya juu na yale ya hali ya chini, na baadhi ya vigezo vingine ambavyo hutumika katika mawasiliano, utamaduni na mgogoro.

Jinsi tunavyoita majina, tunavyopeana lawama na jinsi tunavyotengeneza migogoro hutofautiana kati ya mipaka ya kitamaduni. Kama jinsi mfano wa mzee wa Kichina unavyofafanua, sio kila mtu anakubaliana na mambo yaliyomo katika mgogoro. Kwa wale waliozoea majadiliano ya utulivu, kubadilishana maneno yenye ukali miongoni mwa wanafamilia huonekana na mgogoro unaotisha. Wanafamilia wao wanaweza kuona ni jambo la kawaida na linalokubalika katika kutoa hisia zinazotofautiana. Migogoro yenye kuleta hofu kubwa nayo pia hutafsiriwa kwa hisia tofauti. Je ni tukio lenye kuleta mvutano, uchochezi, kupanda, au jambo dogo tu (hulifananisha na dagaa), ambalo hata halithamaniwi? Jibu litategemea mtazamo, mazingira ya tukio, na namna mhusika anavyohusiana na tukio lenyewe.

Kama vile ambavyo hakuna makubaliano kati ya tamaduni au mahali kwamba ni nini maana kimo ndani ya mgogoro au kwa jinsi gani matukio

katika mahusiano yaandaliwe, hivyo zimekuwepo njia nyingi za kufikiri jinsi ya kukabili ana nayo. Je, kuna umuhimu wale wanaohusika kukutana ana kwa ana, kushirikishana mitazamo yao na visa vyao wakiwa au bila ya msaada wa mpatanishi kutoka nje? Au rafiki anayeaminika azungumze na kila anayehusika na kujaribu kuyapooza maji? Je kuna umuhimu wa rafiki huyo mwingine ajulikane na walengwa au mgeni kwa wanaohusika?

John Paul Lederach, katika kitabu chake kinachojulikana “Kujiandaa kupata Amani: Mabadiliko ya Mgogoro katika Tamaduni”, kinabainisha majukumu mawili yanayomhusu mhusika wa kando ambayo yamo katika mazingira ya mgogoro kati ya Marekani na Somalia, kwa upande mmoja; mpatanishi rasmi na wazee wa jadi kwa upande mwingine. Mpatanishi rasmi kwa ujumla huwa hawajulikani kwa wale wanaohusika, na wao hujaribu kufanya kazi bila upendeleo au kutegemea kupata malipo yoyote kwa lolote litakalotokea. Wazee wa jadi huheshimiwa kwa hekima zao za asili na mahusiano, na hutegemewa katika kuto mwelekeo na ushauri, pamoja na kwa ujuzi wao katika kusaidia kuwashawishi wahusika wawasiliane na wenzao. Baadhi ya majukumu ya mtu wa ndani (ambaye anajulikana na wahusika na anajua historia ya jambo lenyewe na uhusiano uliopo kati ya wahusika) na mtu wa nje ambaye hausiki na upande wowote (ambaye hajulikani na wahusika na hajui lolote litakalotokea au uhusiano uliopo kati ya wahusika) hujitokeza katika mtiririko wa mazingira tofauti ya tamaduni. Kwa ujumla, watu wa ndani ambao hutoa upendeleo kwa mambo yanayohusu utamaduni, hupatikana katika mazingira ya hali ya juu, wakati watu wa nje ambao hawafungamani na upande wowote kwa kawaida hupatikana katika mazingira ya hali ya chini.

Hayo ni baadhi tu ya maeneo ambayo migogoro ya kujitafutia inavyotofautiana kati ya tamaduni mbalimbali. Watu wa kando wanaweza kutumia mbinu na malengo mbalimbali, hii inategemea fikra zao za kitamaduni ni kitu gani kinahitajika. Katika mazingira yaliyotawaliwa na hali zote mbili; ya juu na chini, matarajio ya wahusika kuhusu namna migogoro inavyotakiwa ishughulikiwe hutofautiana, hivyo huzidi kuukuza mgogoro uliopo.

Mbinu zinazotumika kufanya maamuzi pia zinatofautiana kati ya tamaduni mbalimbali. Hampden-Turner na Trompenaars wanabainisha kwamba watu huwa na mitazamo inavyotofautiana katika kuendeleza maisha yao, ikiwa ni pamoja na: ‘wayunivesalisti’ (hupendelea zaidi kanuni, sheria, na mapendekezo ya pamoja); ‘wapatikularisti’ (hupendelea kuhitilafiana, kukabili ana, na tathmini ya mazingira); ‘waspesifisiti’ (hupendelea kutanguliza ufafanuzi usio na utata, kunyambulisha mambo katika sehemu ndogo ndogo na matokeo yanayopimika); ‘wadifyushenisi’ (hutilia mkazo zaidi mifano, ukubwa wa jambo na mchakato wake zaidi ya matokeo); ‘mwelekeo wa ndani’ (hutambua juhudi za watu wanaojitahidi kujikutambua) na ‘mwelekeo wa nje’ (jambo la muhimu liko katika muonekano wa nje wa kila mmoja wetu hii ni pamoja na miondoko ya asili, tabia, uzuri na mahusiano); ‘vinavyotokea kwa wakati mmoja’ (mzunguko na yenye kujiviringa); na wakati uliojipangilia (wa

moja kwa moja au wenye mwelekeo mmoja tu).

Wakati tunapokuwa hatuelewi kuwa watu wengine wanaweza kuwa na mtazamo tofauti kabisa, kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kutokea mgogoro na kusambaa zaidi. Ingawaje mitazamo yenyewe haifungamani na upande wowote, nia mbaya mara nyingi huusishwa na mtu ambaye anaanzisha kutokea kwenye mwisho thabiti.

Kwa mfano, wakati watu wa Mataifa ya Kwanza wapokaa chini na wawakilishi wa serikali kujadili madai ya ardhi nchini Canada au Australia, maoni ya nyakati tofauti yanaweza kuleta ugumu katika kugundua makubaliano yalikuwa nini na kufanya maamuzi. Wakati watu wa Mataifa ya Kwanza huwa na tabia ya kuona wakati kama unanyumbulika kwa kwenda mbele na kurudi nyuma, hivyo kuwalazimisha kuwa na mahusiano na vizazi saba katika mielekeo yote miwili. Matendo yao na uchaguzi wao wa sasa una uhusiano na historia na vizazi vyao. Watu walioziwakilisha Serikali zao katika mazungumzo walibadilika na kuwa na mawazo ya Ulaya ya Magharibi, hivyo kuna wakati wanaweza kujikuta wakisimulia historia na mawazo yanayokadiria kutokea katika vizazi vijavyo katika namna isiyo na maana labda kama wao wataweza kuelewa tofauti ya nyakati kama inavyoeleweka na watu wa Mataifa ya Kwanza.

Bila shaka, mfano huu umechukuliwa katika nadharia ambazo zinaweza au haziwezi kutumika katika hali fulani. Kuna Waaborijino wengi wenye asili tofauti katika nchi za Canada, Australia, New Zealand, Marekani, na mahali pengine. Kila kundi lina utamaduni wa pekee, na hizi tamaduni zina mahusiano tofauti na nyakati, mawazo tofauti kuhusu makubaliano, na utambulisho wa kipekee. Watu wanaoziwakilisha serikali zao wanaweza wakawa na utambulisho wa tamaduni wa aina mbalimbali ambazo hazikubaliani na ubaguzi wa waziwazi wa mwanamke au mwanaume, kwa kutumia vigezo vinavyoshinikizwa na mabadiliko yanayoletwa na nyakati.

Mifano pia inaweza ikatolewa kutoka katika vigezo vingine vitatu kama vilivyoainishwa na Hampden-Turner na Trompenaars. Wakati migogoro inayoweza kuleta hofu kubwa imekuwa ikiendelea kwa takribani miaka mingi au hata vizazi vingi, je kuna haja ya kukimbilia viwango vya kimataifa na wasuluhishi, au kanuni za ndani na mazoea? Wale wanaokubaliana na nadharia ya 'wayunivesalisti' ni wazi kuwa watataka mataifa ya nje yaingilie kati na uanzishwaji wa viwango vya kimataifa. 'Wapatikularisti' watafurahia zaidi kutumia mbinu zilizoandaliwa na wenyewe, mbinu zilizobuniwa na wenyeji kuliko kuanzisha kanuni za jumla ambazo zinaweza au haziwezi kukidhi matakwa yetu na hali ya mazingira.

Hali ya upekee na usambaaji usiokuwa na mpango pia husababisha migogoro hasa migogoro yenye kuweza kuleta hofu kubwa. Watu, ambao huzungumzia mambo maalum, yao pekee, katika harakati za kutafuta ufumbuzi wa changamoto ambazo zinaweza kutekelezwa na kupimwa

matokeo yake, wanaweza kuwaona wale wanaojali zaidi mchakato, hisia, na ukubwa wa jambo lenyewe, kuwa ni wakinzani na wanaowachanganya. Kwa upande mwingine, wale ambao hatua ya kuanzia ni ile ya uenezaji wa taratibu wanaweza kujikuta wanachukulia mambo katika ujumla wake ambayo sio rahisi kuchunguza kwa kuangalia visehemu visehemu, na kuona mazingira ya ndani ambayo mawazo kama hayo yanaweza kufaa.

Watu wenye kuongozwa na dhamira zao huwa na tabia ya kujiamini na kuona kwamba wanao uwezo wa kufanyia marekebisho mabadiliko kwa vile huamini kwamba wao “wana uwezo au nguvu za hatma za maisha yao”, ni viongozi wa roho zao”. Huzingatia zaidi matokeo kuliko mchakato. Hebu fikiria ni kwa kiasi gani wanachanganyikiwa wakati wanapokabiliana na watu wenye kuongozwa na dhamira zao, ambao jambo la muhimu kwao kulinda mahusiano, asili yao kuishi kwa amani, kwenda na hali ilivyo, na kutoa kipaumbele kwa mchakato badala ya matokeo. Kama ilivyo katika kila safu ya hatua ya mambo yaliyotajwa, hakuna aliyesahihi au anayekosea, ni kwamba wanatofautiana tu. Kuzingatia mchakato ni muhimu, lakini isiwe kwamba tumeshindwa kabisa kuyapuuza matokeo. Kuzingatia matokeo ni muhimu, lakini pia ni muhimu kufuatilia ubora na mwelekeo wa mchakato. Fasihi katika utamaduni ni kuwa na ufahamu wa safu za hatua mbalimbali, na kuwa na uwezo wa kuzungumza katika lahaja/lafudhi zote mbili, na kusaidia kuwatafsiria wakati wanapofanya maamuzi ambayo yataufanya mgogoro uwe mbaya zaidi.

Mfululizo wa makala haya si kamili, na wala hayawezi kuelezea mahusiano ya binadamu kwa upana. Ni vidokezo vya nini kinaweza kuwa kinatokea wakati watu wakiwa katika mgogoro kwa muda mrefu. Sisi ni viumbe ambao hutoa tafsiri ya mambo, kusimulia hadithi na kuanzisha maelewano ambayo yatalinda utu wetu na kuyahusisha na makusudio yetu. Tunapokuja kutambua hili, tunaweza kuangalia mchakato wa kufanya maamuzi yenye maana kwa wale walio katika migogoro na kutafuta njia za kuwasaidia waweze kufanya mchakato ya maamuzi yenye maana na misimamo iliyo wazi zaidi kwa kila mmoja.

Hii inaweza kufanyika kwa kusimuliana hadithi na kutengeneza hadithi za pamoja, hadithi ambazo zimetengenezwa kwa kushirikiana zinatoa mwanya kuingizwa kwa mitazamo mbalimbali waliyonayo kila mmoja. Mara nyingi watu walio katika migogoro husimulia hadithi ambazo zinaashiria kwamba wote hawawezi kuwa wakweli. Mbinu za kusaidia kutatua migogoro zinazotumia masimulizi huwasaidia kuwaondolea wasiwasi wao na kuwaacha na wakiwa wamelewa ukweli na kuwa uapnde wenye kufuata haki kwa muda, kugeuza mawazo yao kwenye hadithi ambazo wote wanaweza kuona wao wenyewe.

Njia nyingine ya kuchunguza namna maamuzi yalivyofanywa ni kwa ktumia mafumbo. Mafumbo ni maneno ya mkato yanayokubalika kati ya pande mbili ambayo hutumika katika kufikisha ujumbe au kutoa picha ya hali fulani. Kwa mfano, ukitaka kuchunguza namna mgogoro ulivyoanza, upande mmoja unaweza kutoa maelezo kwamba asili yake imepotelea mawinguni nyakati zilizopita kabla hata ya kuwepo kwa mipaka, barabara na sheria zilizoandikwa. Upande mwingine wanaweza kuelewa kwamba ukoo ule unaleta madai yasiyo na msingi ili kuwasumbua ilianza mwaka 1946. Hakuna aliyekosea, tatizo linaweza kuwa na mizizi ya ndani, na madai yaliyotolewa yanaweza kuwa ndio chanzo cha mgogoro. Jinsi pande mbili zinavyozidi kutoa mafumbo yao, ndivyo wanavyozidi kueneza na kusambaza ukweli hasa ulijioficha katika nyakati zilizopita, ambao umejikita katika uamuzi fulani wa kisheria. Pande hizi mbili zikizidi kujadiliana, huimarisha uelewano wao halisi, na kujifunza zaidi kwamba majukumu ni yapi na kuelewa utambulisho wao.

Utambulisho na majukumu humaanisha kujitambua. Je mimi ni kitengo cha binafsi, niko huru, wakala wa kujitegemea, ninayejiwajibisha mimi mwenyewe? Au ni ntu wa kwanza au mwanachama anayetangulizwa katika kikundi, kupima uzito wa athari zitakazokikuta kikundi kutokana na chaguzi na matendo yake. Wale wanaojitenga na kufanya mambo peke yao mmoja mmoja kuna uwezekano waanthropolojia wakawaita wabinafsi. Wale ambao masuala ya kikundi ni kitu cha msingi kwao mara nyingi hutokea katika mazingira ambayo waanthropolojia huyaita 'wajamaa' (mfumo wa uchumi ambamo rasilimali humilikiwa na umma) au wakomunisti.

Katika mazingira ya kijamaa, maadili yafuatayo hupewa upendeleo maalum:

- (i) Ushirikiano;
- (ii) Uchaji wa Mungu (heshima na staha mbele ya wazee);
- (iii) Kushirikiana katika maendeleo ya pamoja;
- (iv) Sifa ya kikundi/umoja; na
- (v) Kutegemeana.

Katika mazingira ya ubinafsi, maadili yafuatayo hupewa upendeleo maalum:

- (i) Ushindani;
- (ii) Uhuru;
- (iii) Mafanikio ya ntu binafsi;
- (iv) Ukuaji na utimilifu wa mtu binafsi;
- (v) Kujitegemea;

Wakati hatua za kuanzia maisha za wabinafsi na wakomunisti zinapofanikiwa kuwashawishi wale ambao hawako katika upande wowote wa mgogoro, uvunjifu wa amani unaweza kujitokeza. Wanaoamini ubinafsi wanaweza kuona kwamba hakuna tatizo kupambano "huwezi kuzuiliwa kuchukua hatua yoyote ile ili kupata unachotaka", wakati wakomunisti

wenzao wao hujishusha na kuacha kutenda matendo ambayo wanajua yataleta aibu au hasara ya wazi katika kikundi chao na hivyo kutenda mambo kimya kimya kwa njia ya adabu. Wanaoamini ubinafsi wanaweza kuamini kwamba wamefanya mkataba na wakomunisti, lakini wakastukia wamegeukwa wanapogundua kuwa wenzao wametoa msimamo wao hadharani juu ya mambo ambayo wanajua yataathiri kundi kubwa kabla ya kufikia mwisho. Mwishoni, inabidi kila mmoja akumbuke kwamba kama ilivyoelezewa katika mifumo mingine, watu wengi sio kwamba wabinafsi au wakomunisti safi/halisi. Badala yake, watu wanaweza kufanya ubinafsi au ukomunisti hatua ya kuanzia, kutegemeana jinsi mtu alivyolelewa, uzoefu na hali halisi ya jambo lenyewe.

Hitimisho

Hakuna mbinu ya aina moja tu ambayo itafaa kutatua mgogoro, hii ni inatokana na sababu kwamba utamaduni mara zote ni moja ya mambo yanayochangia. Kwa hiyo fasihi katiika utamaduni ni jambo wanalolitumia sana watatuzi wa migogoro au kama mtu anataka kuleta mafanikio sehemu mbalimbali na maisha yao. Fasihi katika utamaduni inahusu kujitambua na kuishi maisha ya adabu kufuatana na uelewa kwamba mawasiliano, namna tunavyoita majina, utungaji, na namna tunavyoita futa migogoro, tunavyoimaanisha mambo, utambulisho na majukumu hutofautiana kati ya utamaduni mmoja na mwingine.

Chanzo:

<http://www.beyondintractability.org/action/essay.jsp?id=26234&nid=1186>

Wasifu

Toleo la Kwanza: Juni 2009 kama ilivyoandaliwa na Anna Hoppenau na Johannes Hahn

Mwongozo huu wa utamaduni unatakiwa kukua na kuendelezwa zaidi. Kwa hiyo uwe huru kutuma maoni au mapendekezo uliyonayo kupitia barua pepe hii info@d-t-p-ev.org au kuomba utumiwe nakala yake ili uifanyie marekebisho wewe mwenyewe. Lakini usisahau kuituma tena kwetu! Asante.

Chanzo cha Mrejeo

Ukurasa wa 4:

<http://en.wikipedia.org/wiki/culture>

www.umanitoba.ca/faculties/arts/anthropology/courses/122/module1/culture.html

Ukurasa wa 7:

<http://en.wikipedia.org/wiki/Collectivism>

<http://en.wikipedia.org/wiki/Individualism>

Ukurasa wa 12:

http://en.wikipedia.org/wiki/Culture_shock

Picture and text: http://www.isc.sdsu.edu/study_abroad/accepted-culture-shock.html

Ukurasa wa 13:

Drawn and slightly adapted from: <http://www.artsci.utoronto.ca/prospective/contact-us/cristian-test-page/>

Ukurasa wa 14-15:

<http://en.wikipedia.org/wiki/Stereotype>

<http://en.wikipedia.org/wiki/Prejudice>

Alan McGregor: "The double nature of prejudice",

<http://es.geocities.com/sucellus24/2061.htm>

Ukurasa wa 16:

Ilitafsiriwa na kuchukua maana kutoka: <http://www.kwintessential.co.uk/cultural-services/articles/intercultural-communication-tips.html>

Ukurasa wa 17:

[http://www.roshan-](http://www.roshan-institute.org/templates/System/details.asp?id=39783&PID=474552)

[institute.org/templates/System/details.asp?id=39783&PID=474552](http://www.roshan-institute.org/templates/System/details.asp?id=39783&PID=474552)

Pages 18-20:

www.umanitoba.ca/faculties/arts/anthropology/courses/122/module1/culture.html

Ukurasa wa 21:

Picture: <http://bohemica.com/czechcultureguide/aboutculture/definitionsculture>

Ukurasa wa 23-27:

<http://www.beyondintractability.org/action/essay.jsp?id=26234&nid=1186>